Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

# Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 74 No. 176 | SHAWWAL 1434 AH | AGOSTI 2013 | ZAHOOR 1392 HS | BEI TSH. 500/=

**Nukuu ya Qur'an Tukufu**

**Mwenyezi Mungu Amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, bila shaka Atawafanya makhalifa katika ardhi kama Alivyowafanya makhalifa wale wa kabla yao, na kwa yakini Atawaimari-shia dini yao Aliyowapendelea, na Atawabadilishia amani baada ya hofu yao. Wataniabudu, hawatanishirikisha na cho chote. Na atakayekufuru baada ya hayo, basi hao ndio wavunjao amri. (24:56)**

## Jalsa Salana ya 47 Uingereza yapata mafanikio

# Watu zaidi ya 30,000 wahudhuria 540,000 wajiunga na Jumuiya, tafsiri za Qurani zafikia lugha 71

**Na Mwandishi Wetu**

Mkutano wa 47 wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Uingereza, ambao pia unabeba sura ya kimataifa kwa kuwepo *Khalifatul Masih* (Kiongozi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya duniani Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a) pamoja nao, umefanyika kwenye tarehe 30, 31 Agosti na tarehe 1 Sept. 2013, kwenye viwanja vya Hadeeqatul Mahdi huko Oaklands Farm, Alton. Zaidi ya washiriki 30,000 kutoka mataifa mbalimbali duniani wamehudhuria mkutano huo.

Mwaka huu Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Uingereza iliadhimisha pia karne moja tangu Jumuiya ilipoingia nchini humo.

Katika siku ya kwanza ya Jalsa Salana hiyo, *Khalifatul Masih a.t.b.a.* alitoa hotuba mbili. Ya kwanza ilikuwa ni hotuba ya

*Endelea uk. 3*



*Kiongozi wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya duniani, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (a.t.b.a), akiongoza maombi ya kufunga Jalsa Salana ya Uingereza 2013*

# Ndoto 3 tukufu za Mtume Muhammad s.aw

**Ustadhi *A .R. Mikila – Morogoro***

***Kwa jina la Allah, Mwingi wa Rehema Mwingi wa Ukarimu.***

Makala hii inakusudia kuzungumzia habari za ndoto tatu tukufu za Mtume Muhammad (saw), ambazo aliwahi kuziota wakati wa uhai wake hapa duniani. Ndoto hizo ni ile **Safari ya Mi'raji**, **Safari ya Isra na safari ya Kutufu Kaaba**. Nimezichagua ndoto hizi kwa sababu maalum. Kwanza ni kwa sababu, ndoto hizi ni maarufu sana katika ulimwengu wa kiislamu. Pili ni kwa sababu zimeleta mgawanyiko mkubwa miongoni mwa waislamu katika kuzifamu hakika zake. Tatu, ni kwa sababu matukio yaliyo ambatana na ndoto hizi, na zile taathira chanya zilizo patikana katika maendeleo ya dini ya kiislam katika uhai wa Mtume (saw).

**NDOTO NI NINI?**

Ndoto ni ile hali ambayo, mtu awapo usingizini, anajiona kama vile yupo macho. Anatembea, anaongea, anakula, anakunywa na hata kujiona anafanya kazi nyingi mbali mbali. Ndotoni anajiona anakukutana na watu anowajua na asiyo wajua; wakiwemo hata wale waliokufa zamani. Pengine hujiona yupo msituni, baharini au mtoni akioga na kuogelea. Kwa mantiki hiyo ndiyo maana, tangu zamani ndoto zilifahamika na kusimuliwa na watu mbali mbali.Tangu kale hadi leo, ndoto zimekuwa ni moja ya njia ghaibu ya mawasiliano ambayo, Mwenyezi Mungu huitumia kuwasiliana na waja wake kwa nia ya kuwajulisha kile wasicho kijua au kile ambacho waja hao, wanatamani kukijua kwa kukifanyia bidii sana. Mawasiliano haya ya ghaibu kati ya Allah na waja wake ndiyo chanzo kilichozaa maarifa mengi ya uvumbuzi na elimu mbali mbali za matumizi ya vitu vilivyopo hapa ulimwenguni.

Uvumbuzi wa kamera, picha za mnato, runinga, simu za upepo, simu za mezani na simu za mkononi, vyote hivyo na vingine vingi vyanzo vya kuvumbuliwa kwake ni ndoto. Leo tunazo barua pepe na vyombo kadhaa vya mawasiliano, tunavyo vyombo

*Endelea uk. 4*

# Hekima ya mavazi mapya katika sherehe ya Idi

**Ally Khamis Mbambwa, Dar es Salaam**

Kwa fadhila na Rehema za Allah,tumemaliza Mfungo wa mwezi mtukufu wa Ramadhani kwa kusherehekea kwa ibada ya sala ya idd,kula na kunywa pamoja na mavazi mazuri, ALHAMDDULILLAH. Naamini sawa na mazingatio yaliyoainishwa ndani ya Qur'an Tukufu juu ya mwezi wa Ramadhani, bila shaka kwa wazingatiao wanalo chumo kubwa la masurufu ya Taqwa yatakayoweza kuwafaa kwa mwaka mzima ujao Insallah.

Ni ada toka azali katika jamii ya kiislam hususan inapokaribia sikukuu ya iddil-fitri ambayo hutanguliwa na mwezi mtukufu wa Ramadhani kuwaona wazazi wakifanya jitihada za makusudi kuhakikisha chakula kizuri kinapatikana kwa ajili ya kusherehekea sikukuu hiyo. Halikadhalika mavazi huwa ni jambo linalopewa umuhimu wa pekee. Ni nadra sana kumkuta mtoto wa kiislam katika sikukuu hii kukosa vazi jipya. Na hata kama litakuwa sio jipya basi huwa ni vazi maridadi lililohifadhiwa kuvaliwa siku hiyo iliyo kuu. Kina mama ambao kwa desturi huwa karibu na watoto, huwa wako tayari kuweka rehani vito vyao ili wanawao wapate nguo mpya. Hakika ni jambo linalopendeza sana kuona wazazi wanavyofanya jitihada kuhakikisha muonekano mzuri wa watoto wao.

Hebu tujiulize kidogo!, mavazi mapya na sikukuu hii yanauhusiano gani?. Maana kwa yeyote anayeishi miji mikubwa kama jiji la Dar es

*Endelea uk. 2*

# Mapenzi ya Mungu

## Maoni ya Mhariri

# NURUYADUNIA

**Binadamu pekee aliyeletwa na Allah ili amfikishe katika kilele cha sababu ya kuumbwa kwake ni Mtukufu Mtume Muhammad (saw). Ni yeye aliyekuja na dini iliyokamilika na mafundisho yaliyokamilika. Dunia imechelewa sana kupiga hatua ya kwenda mbele kwa sababu ya kutozingatia mafundisho aliyoyaleta.**

**Ni lazima ikumbukwe ya kwamba dini ya Islam inaamini ya kwamba hakuna kabila wala watu isipokuwa alipita Nabii miongoni mwao akiwaeleza umoja wa Mwenyezi Mungu na sawa na haja ya wakati. Manabii kama walivyotangaza wenyewe walitumwa kwa makabila yao, mikoa yao na wilaya zao. Hali halisi haikuruhusu kuwa na nabii kwa ajili ya dunia nzima. Kwani vikwazo vingi vya usafiri vilizuia uwezekano wa kupita huku na huko.**

**Kudhuhiri kwa Mtukufu Mtume Muhammad (saw) kulikamilisha ile subira au lile jengo lililokuwa zuri na la kuvutia, lakini lilikosa tofari moja ili kukamilisha jengo lenyewe. Kuja kwake akiwa na lugha ya Kiarabu ambayo imethibitishwa kuwa mama wa lugha zote, sifa ya kuwa Nabii kwa ajili ya dunia ikakamilika katika maisha ya Mtukufu Mtume Muhammad (saw) hivyo akachuma sifa ya kuwa mfano kwa ajili ya binadamu wote.**

**Kama Allah Amemkadiria Mtukufu Mtume (saw) kuwa muonesha njia, mfano bora kwa wengine, anayefaa kufuatwa na kutiiwa, kosa ni la nani basi tunapokumbana na mikasa na matatizo ambayo tunayo hivi sasa? Kwa unyenyekevu mkubwa sana tunaomba msikilize sauti inayowaita kufuata na kumsaidia Mtume huyu Mtukufu ili bendera ya heshima Mtume Mtukufu (saw) iweze kupepea duniani kote.**

**Wakati umefika tuache kichwa ngumu, tuache kiburi, tuache majivuno, kwani anguko la Ibilisi lilitokana na sifa hizo. Mateso makubwa yanayoendelea Syria hivi sasa yanaumiza kila roho ya m tu ambaye anaamini kwamba kuuawa kwa mtu mmoja ni kana kwamba umeua dunia nzima. Dunia haiwezi kuendelea kusimama ikitizama watu wa Syria wanavyoangamizwa. Upo wajibu mkubwa wa kuacha kufanya ukaramsi wa kitoto na h ivyo kutafuta ufumbuzi wa tatizo hilo kutoka mafundisho ya Mtukufu Mtume Muhamamd (saw). Na ni katika mafundisho yake tu ndipo tunapoweza kupata suluhisho la mgogoro wa Syria.**

**Islam inatangaza tena bayana kwamba Muislam ni ndugu ya Muislam mwingine, inakuwaje basi Muislam anadiriki kutumia silaha tena silaha kali katika kumuangamiza nduguye Muislamu? Ni msiba mzito kiasi gani mtu anaumwa tena anaumwa sana, anapewa dawa naye anasema ya kwamba haitamani dawa hiyo! Khalifa wa Mwenyezi Mungu Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (atba) ameshaeleza ya kwamba tiba ya matatizo yote yaliyomo duniani kwa hivi sasa yatatokana tu kwa kufuata si kwa maneno bali kwa vitendo mafundisho ya Mtukufu Mtume Muhammad (saw) kwani ndiye aliyekuja na tiba ya kutibu maradhi yote ya mwanadamu.**

**Maradhi kama vita, unyonyaji, unyanyasaji haya yote ameyaletea tiba. Dunia yote tunawaita kwa mbora wa viumbe vyote Khataman Nabiyyina ili mpate tiba.**

**Na hutokuta mabadiliko katika mwenendo wa Mwenyezi Mungu, penye maradhi ya kiroho daima hutuma daktari wa kiroho, hapo ndipo inadhihirika nafasi, makusudi, shabaha, na wajibu wa Jumuiya ya Waislam wa Ahmadiyya. Hili ni jeshi la Mtukufu Mtume Muhammad (saw) Amir jeshi wake ni Masihi Aliyeahidiwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as). Jeshi hili la kiroho lina wajibu wa kudhihirisha kwa mara ya pili kwamba uzima wetu, maisha yetu, kifo chetu ni kwa ajili ya kueneza mafundisho matukufu ya Kurani Tukufu. Ni sisi wa kueneza mafundisho hayo sahihi kama yalivyooneshwa na Mtukufu Mtume (saw). Ni sisi wa kulinda, kutetea heshima ya Mtukufu Mtume Muhammad (saw), si wajibu mdogo. Tunakuomba Mola wetu Utuwezeshe kutawanya vidonge hivi vya kiroho ili dunia iliyo taabani iweze kupona na kushiriki katika kukuabudu Muumbaji wa mbingu na ardhi na kumtakia amani na rehema Mbora wa viumbe wote Mtukufu Mtume Muhammad (saw) - Amani na rehema za Allah ziwe juu yake.**

# Hekima ya mavazi mapya katika sherehe ya Idi

*Kutoka uk. 1*

salaam alijiuliza swali hili pale alipoathiriwa kwa namna moja au nyingine na wimbi la watu waliovamia maeneo mbalimbali kwa ajili ya kuhakikisha nguo mpya zinapatikana.Wiki moja kabla ya Sikukuu, hali ya usafiri katika jiji hili ilikuwa ni tafrani tupu. Vituo vilijaa watu toka asubuhi hadi jioni,misururu ya magari ilikuwa haisemeki barabarani. Umati uliokuwepo Kariakoo ulishindana na ule wa Tandika. Ukienda Mbagala utadhani watu wote wamehamia huko, Mwenge ,Buguruni, na sehemu nyingine kadhaa ilikuwa ni mafuriko ya watu. Chanzo, watu kusaka nguo za Sikukuu.

Kabla sijaelezea uhusiano wa nguo na Iddil fitri, tuangalie sababu za kuvaa nguo na umuhimu wake.

Katika mahitaji ya msingi ya mwanadamu ni pamoja na mavazi. Mavazi yameambatana na historia ya mwanadamu tangu alipoanza kujitambua. Kabla ya maendeleo na uvumbuzi wa mavazi ya kitambaa, mwanadamu alitumia mavazi ya magome ya miti, majani na hata ngozi za wanyama kujihifadhi . Madhumuni makubwa yakiwa ni kuhifadhi utupu wake, kujikinga na baridi, miali ya jua pamoja na moto. kujilinda kung'atwa na wadudu kwa kuweka ulinzi baina ya ngozi na vilivyo mzunguuka n.k. Mavazi pia yalitumika kutambulisha jinsia, taaluma, na hata Dini. Mavazi yalitumika kujipamba na pia kama nembo ya kuitambulisha jamii na utamaduni wake. Hali kadhalika hata jamii ya leo iliyopiga hatua ya maendeleo, zaidi ya kugundua vazi la kitambaa, haitoki nje ya duara hili la matumizi ya mavazi ambalo ndilo jambo la msingi na la muhimu. Kwa neno zima juu ya umuhimu wa mavazi kwa mwanadamu umeanishwa vizuri sana na Qur'an Tukuku kwa dafaa yake moja tu pale Allah aliposema *" Enyi wanadamu,hakika tumewateremshieni nguo zifichazo aibu zenu na mapambo….."*(7:27). Katika jiografia ya Dunia, popote mtu alipo kama hatovaa nguo, bila shaka ataaibika. Na kama atajipamba sawa na utamaduni wake atapambika. Mambo mengine yanategemea hali ya hewa na mazingira ya eneo. Kwa sababu wako watu wanavaa nguo nzito kujikinga na baridi, na sehemu nyingine hulazimika kupunguza nguo kwa sababu ya joto. Halikadhalika kujilinda na wadudu inategemea na mahali ulipo. Kwa neno zima sababu za kuvaa nguo ni kuficha, kustiri na kuhifadhi aibu zetu pamoja na kujipamba .Na kama hatutovaa nguo, matokeo yatakuwa ni kinyume chake kwamba tutafedheheka na kuaibika, hatutositirika wala kutopendeza mbele ya jamii.



**Ally Khamis Mbambwa,**

Tukirudi katika somo letu la msingi napenda nieleze mahusiano yaliyopo juu ya mavazi na sikukuu ya iddil-fitri kama ifuatavyo.

Awali ya yote yatupasa tufahamu kinaga ubaga maana ya Iddil-fitri, halafu uhusiano wa mavazi na sikukuu hii bila shaka utatubainikia. Tukianza na neno **'IDD** linatokana na mzizi wa neno la kiarabu 'ADA linalomaanisha ***kurejea*** au ***kurudia kwa kitu au jambo.*** Hivyo tunaposema Yaumul 'idd, tunamaanisha Siku kuu inayo jirudiarudia. Na ni kweli kabisa maana hii ndio tunayoishuhudia kila mwaka siku hii ikijirudiarudia. Na neno FITRI linatokana na mzizi wa neno **FATWARA** lenye maana ya ***kukata kitu au jambo, kuanzisha, asili ya kitu*** au ***upya wa kitu.*** Hivyo tunaposema IDDIL-FITRI, tunamaanisha sikukuu inayojirudia ambayo kila kitu hurudishwa katika asili yake, ni siku ya kufanya upya jambo au ni siku ya kuanza jambo mwanzo kabisa. Kwa muktadha huu, kwa kuwa sikukuu hii inawahusu binadamu, hapa itamaanisha kuwa ni siku kuu ya mtu kufanywa mpya,kurudishwa katika asili yake aliyozaliwa nayo.Na asili ya mwanadamu imeelezwa na Mtume Mtukufu Muhammad (s.a.w) kuwa *"ma min mauluudin illa yuulad 'alal fitrat, fa-abawaahu yuhawwidaanihi, au yunaswiraanihi au Yumajjisaanihi"* ). Yaani, kila mtoto huzaliwa katika asili , ama wazazi wake watamfanya myahudi,mnaswara au mmajusi. Hadithi hii inatufahamisha kuwa hakuna mtoto anaezaliwa na dhambi au makosa. bali kila mtoto azaliwae huwa yu safi na salama kabisa bali miongozo na malezi ya wazazi wake ndio yanayoweza kumpoteza mtoto akajikuta amefuata mifumo ya kiyahudi, kinaswara au kimajusi. Hivyo Sikukuu ya Idd ni siku inayotufanya turudie katika asili yetu yaani kutokuwa na dhambi wala makosa. Mtume Mtukufu (SWA) alielekeza njia kadhaa za kufuata ili mtu arejee katika asili yake, mojawapo ni pale atakapotekeleza kikamilifu saumu ya mwezi mtukufu wa Ramadhani. Mtume Mtukufu Muhammad (s.a.w) amesema *"Afungae saumu katika mwezi wa Ramadhani kwa imani na nia njema atasamehewa madhambi yake yote yaliyotangalia"* (Bukhari na muslim). Na katika hadithi nyingine Mtume (SAW) amesema *" Watu watatu ni wenye bahati mbaya, mmojawapo ni Yule ambae Mwezi wa Ramadhani umemkuta na hakusamehewa dhambi zake……"* (Bukhari na Muslim).

Baada ya maana hii ya iddil-fitri tuliyoipata, tuinasibishe sasa na mavazi mapya yanayovaliwa siku hiyo. Hapo kabla nilieleza kwa mapana sababu na umuhimu wa kuvaa nguo. Nikasema sababu kubwa ni kusetiri aibu zetu pamoja na mapambo. Lakini aya ile iliyotoa maelezo hayo inaendelea kwa kuelezea jambo la msingi zaidi pale Allah (SW) aliposema *" Enyi mlioamini, tumekuteremshieni nguo zifichazo aibu zenu na mapambo; na nguo za utawa ndizo bora…."* (7:27). Kwa kuongezea kifungu hiki cha aya hii Allah (SW) anatufahamisha umuhimu ulio mkubwa sana wa kuvaa mavazi. *LIBASU TAQWA* yaani VAZI LA UCHAMUNGU ni vazi la kiroho ambalo mwanadamu anapaswa alivae katika maisha yake. Kama vile mtu anavyo vaa vazi la kidhahiri kwa ajili ya kumsitiri mwili, basi yampasa pia avae vazi la kiroho ambalo litastiri khulka na mwenendo wake. Na vazi hilo la kiroho linapatikana kwa wingi kwa kufanya ibada ambazo hufanywa kwa wingi sana kuliko wakati wowote katika mwezi mtukufu wa Ramadhani. Kwa sababu Mtume Muhammad (SAW) alisema, atakaefunga mwezi wa Ramadhani na pia akafuatisha

***Endelea uk. 7***

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jumuiya, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Abdurahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Muhammad Arif
Msambazaji: Mwl. Omar Mnungu
Wajumbe: 1. Abdullah Khamis Mbanga
2. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jumuiya Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu@yahoo.com

# Jalsa Salana Uingereza 2013 yapata mafanikio

*Kutoka uk. 1*

Ijumaa na baadae hotuba ya ufunguzi wa Jalsa hiyo. Kama ishara ya kufungua rasmi Jalsa hiyo *Khalifatul Masih a.t.b.a.* alipandisha bendera ya Jumuiya sambamba na upandishwaji wa bendera ya Taifa la Uingereza mbele ya bendera zingine za nchi mbalimbali duniani.

Katika hotuba yake ya Ijumaa, *Khalifatul Masih a.t.b.a.* alizungumzia juu ya lengo la Jalsa Salana. Alisema kwamba Jalsa Salana si tukio la kisiasi bali ni tukio lenye uhalisia wa kiroho pekee kwa lengo la kutoa nafasi ya kuleta mabadiliko ya kimatendo na kitabia kwa wahudhuriaji ikiwa ni jitihada ya kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu.

Katika hotuba yake rasmi ya ufunguzi wa Jalsa hiyo, *Khalifatul Masih a.t.b.a.* alizungumzia jinsi Mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Hazrat Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian a.s., alivyotumwa kwa lengo la kuiangazia dunia juu ya mafundisho sahihi ya Islam yenye kuleta amani ya kweli. Alisisitiza kwamba Masihi Aliyeahidiwa a.s. daima aliwataka wafuasi wake kuonyesha kiwango cha hali ya juu cha imani yao kwa Mwenyezi Mungu sio kwa maneno tu bali hasa kimatendo.



*Khalifa Mtukufu V a.t.b.a. akifanya maombi baada ya upandishaji wa bendera ya Jumuiya sambamba na bendera ya taifa la Uingereza.*



*Khalifa Mtukufu V a.t.b.a. akiwaaga washiriki wa Jalsa Salana ya Uingereza 2013 baada ya kufanya maombi ya ufungaji wa Jalsa hiyo*



*Sehemu ya wasikilizaji kwenye Jalsa Salana ya Uingereza 2013*

Hadhrat Khalifatul Masih a.t.b.a. alisema kwamba kiini cha mafundisho ya Islam ni kuwahudumia wanadamu. Alisisitiza kwamba ni jukumu la kila mwislamu wa kweli kutimiza haki za wengine badala ya muda wote kujali haki zake tu. Alisema kwamba Masihi Aliyeahidiwa a.s. ametufunza kuwa moyo wa muislam unatakiwa daima ujawe na mapenzi kwa wanadamu.

Akizungumzia juu ya maadhimisho ya karne moja ya Jumuiya ya Waislamu ya Ahmadiyya nchini Uingereza, *Khalifatul Masih a.t.b.a.* alisema:

"***Mwaka huu tunaadhimisha miaka 100 tangu kuwepo kwa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya hapa Uingereza. Ingawaje tuelewe kwamba maadhimisho haya yatakuwa na maana tu na yatakuwa ni sababu ya kweli ya kuleta furaha iwapo miaka hii 100 itakuwa imeleta mapinduzi ya kweli ya kiroho miongoni mwetu na ambayo yataendelea pia katika vizazi vyetu vijavyo.***"

*Hadhrat Khalifatul Masih a.t.b.a.* alimalizia hotuba yake hiyo kwa kuombea amani ya dunia. Akasema kwamba migogoro katika sehemu mbalimbali za dunia inazidi kuongezeka siku hadi siku na hivyo kupelekea vita vyenye madhara makubwa. Aliziasa sehemu husika kwenye migogoro hiyo, kushika adili katika kutimiza haki za wengine.

Siku ya Pili ya Jalsa, wakati *Khalifatul Masih a.t.b.a.* akitoa hotuba ya kuongeza imani kwenye mkutano huo, alisema kwamba jumla ya watu 540,000 wamejiunga na Jumuiya katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita. *Khalifatul Masih a.t.b.a.* alitoa kauli hiyo wakati akitoa taarifa na takwimu mbalimbali juu ya shughuli mbalimbali za Jumuiya duniani kwa kipindi cha mwaka uliopita.

*Hadhrat Khalifatul Masih a.t.b.a.* pia aliwaeleza wanajumuiya kwamba hadi sasa Jumuiya imeshastawi kwenye nchi 204 duniani. Kwa mwaka uliopita Jumuiya imefika kwenye nchi zingine mbili - Costa Rica na Montenegro.

Zaidi ya hayo *Hadhrat Khalifatul Masih a.t.b.a.* alieleza kwamba kwa kipindi cha mwaka mmoja uliopita Jumuiya imejenga au kupewa jumla ya misikiti 394. Misikiti hiyo inaingiza ile mikubwa ya Canada, Ujerumani na Uhispania ambayo *Hadhrat Khalifatul Masih a.t.b.a.* mwenyewe alihudhuria kwenye ufunguzi. Jumuiya pia imepata jumla ya nyumba za wabashiri 121 duniani kote kwa kipindi cha mwaka mmoja uliopita.

Pia *Hadhrat Khalifatul Masih a.t.b.a.* alitangaza kwamba kama njia ya kuitumikia Islam, Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya sasa imefikia kutafsiri Quran Tukufu kwa lugha 71 za dunia, ya 71 ikiwa ni tafsiri kwa lugha ya Kiyao (kinachoongelewa sehemu za Kusini magharibi ya Tanzania, Kaskazini ya Malawi na sehemu zingine za Msumbiji na Zambia).

Kama njia ya kuwatumikia wanadamu na ubinadamu Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya inazidi kukunjua mikono yake katika kusaidia miradi ya maendeleo kwenye sehemu mbalimbali za dunia.

*Hadhrat Khalifatul Masih a.t.b.a.* alitaja hasa mradi wa 'Maji ni Uhai', ambao unalega kuwapatia maji safi na salama maelfu ya wakazi wa sehemu za dunia ambazo zina shida kubwa ya maji hasa Afrika.

*Hadhrat Khalifatul Masih a.t.b.a.* akataja kwamba huduma hizo ni muhimu kwa ajili ya kuwaopoa wale walionaswa kwenye tatizo kubwa la uhaba wa maji.

Akiongea upande wa ukumbi wa akinamama (Lajna Imaillah) *Hadhrat Khalifatul Masih a.t.b.a.* alisema kwamba watu wa kada mbalimbali kutoka sehemu zote za dunia wanakimbilia kujiunga na Masihi Aliyeahidiwa a.s. kwa njia hii Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya inawaunganisha wanadamu kwenye umoja wenye amani na utulivu.

Hivyo *Hadhrat Khalifatul Masih a.t.b.a.* akasema kwamba uadilifu katika ngazi zote za maisha ni jambo muhimu sana na iwapo tunataka kufikia amani katika jamii, amani hiyo ni lazima ianzie katika ngazi ya familia: Alisema:

"***Ni uzoefu wangu kwamba sababu kuu ya kuvunjika kwa ndoa nyingi ni uchoyo na ubinafsi uliopita kiasi. Ukweli ni kwamba iwapo mume na mke watatendeana kwa usawa na uadilifu, basi hakutokuwa na sababu ya migongano. Kwa hakika amani na uzuri wa jamii yoyote unategemea sana kiwango cha uadilifu na uaminifu uonyeshwao katika kila ngazi..***"

Tukio la kuchangamsha imani la Baiat ya Kimataifa lilifanyika siku ya tatu ya Jalsa hiyo, ambapo *Hadhrat Khalifatul Masih a.t.b.a.* mbali ya kuchukua baiat ya wanajumuiya wapya waliohudhuria kwenye Jalsa hiyo aliwoangoza pia mamilioni ya wanajumuiya duniani waliokuwepo mkutanoni na kupitia MTA kujadidisha baiat zao sambamba na agizo la Mtukufu Mtume s.a.w. alilotuagiza kwamba atakapokuja Masihi Aliyeahidiwa a.s. tuhakikishe tunafanya baiat kwake hata kama itatubidi kutambaa juu ya theluji.

Katika hotuba yake ya ufungaji *Hadhrat Khalifatul Masih a.t.b.a.* alizungumzia juu ya sifa za Muislamu wa kweli.

*Hadhrat Khalifatul Masih a.t.b.a.* akasema Muislamu wa kweli ni yule anayemwamini Mwenyezi Mungu na kudhihirisha imani yake kwa kufanya matendo mema na kisha kuwaita wengine kwa Mwenyezi Mungu (kufanya Tabligh). *Hadhrat Khalifatul Masih a.t.b.a.* akasema kama leo liko kundi miongoni mwa Waislamu linalodhihirisha sifa hizi za musilamu wa kweli basi kundi hilo si jingine zaidi ya Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya pekee.

Kama ishara ya kufungwa kwa Jalsa hiyo, *Hadhrat Khalifatul Masih a.t.b.a.* aliongoza maombi ya kimya kimya yaliyowashirkisha Waahmadiyya duniani kote.

Kwa fadhili za Mwenyezi Mungu vikao vyote vya Jalsa Salana hiyo na matukio yote mengine yalionyeshwa moja kwa moja kupitia MTA na pia mawasiliano yaliweza kupatikana kwa njia ya intaneti kupitia MTA.tv.

# Ndoto 3 tukufu za Mtume Muhammad s.a.w

*Kutoka uk. 1*

kadhaa vya usafiri wa nchi kavu, majini na wa angani, pia tunavyo vyombo vingi vya matumizi ya majumbani mwetu na vya maofisini. Vyote hivyo vilivumbuliwa baada ya watu wakale kuvisimulia kwa namna ya hadithi kutokana na ndoto walizo oteshwa.

Leo zile safari za kwenda kwa miguu kwa umbali mrefu na mfupi, zile barua za kusalimiana na za kupeana taarifa za misiba ndoa na unyago, yote hayo yamebaki kuwa hadithi tu. Wengi wetu leo tunawasiliana kwa mitandao ya simu, sms na barua pepe. Leo tunasafiri kwa Magari, Treni, Meli za mwendo kasi na Ndege. Safari za masafa marefu tunaenda kwa muda mfupi. Dunia imethibitisha ukweli wa ndoto zile, ambazo hapo kale zilisimuliwa kama hadithi za babu na mjukuu. Kutoka katika ndoto zile, leo ulimwengu ume vumbua nyenzo kadhaa za vitendea kazi vya kukuza uchumi, zana bora za vita na mitambo mikukubwa ya kuchimba madini na mafuta. Katika kila Nyanja ya mahitaji ya binadamu mambo yamerahisika sana. Chanzo cha yote hayo ni elimu iliyo anzia kwenye ndoto.

Ni vizuri ifahamike wazi kwamba, binadamu bado anatamani kupata maendeleo na bado anatamani kuendelea kuvumbua mengi ya kumfaa. Bado anatamani kuwa na nyezo nyingi za kumrahisishia kufanya kazi zake za kila siku. Kwa sababu hiyo ni dhahiri kwamba, mawasiliano haya ya ghaibu kutoka kwa Allah Aliye mmiliki Mkuu wa ndoto za uvumbuzi na ujuzi, bado ni muhimu na yanahitajika sana. Qur'an Tukufu inasema:-

"…wala hampasi Mwenyezi Mungu kuwajulisheni *nyote* mambo ya ghaibu, baliMwenyezi Mungu humchagua katika Mitume wake Amtakaye *akamjulisha.* Basi mwaminini Mwenyezi Mungu na Mitume Wake..."Kur 3:180

### NDOTO ZA MITUME NA VIONGOZI WA KIJAMII

Wachamungu na viongozi wa Kijamii, kadhalika viongozi wa nchi, aghalabu huoteshwa ndoto za uongozi, sawa na mazingira yao na kazi zao. Ndoto za viongozi hawa na za wale watu maarufu miongoni mwa jamii, zilichukuliwa kuwa, ni kauli ghaibu itokayo kwa Allah, kwa sababu tabiri zao zilikuja tokea kuwa kweli. Kutimia kwa mambo yaliyo tabiriwa kulizaa ufatiliaji wa habari za ndoto na matokeo ya ndoto hizo.

Watu wa kale waliushikilia utamaduni huu na kuuendeleza sana. Ndoto zikapata nguvu ya kuaminiwa sana hasa pale mfasiri wa ndoto anapo kuwa ni kiongozi Mcha Mungu na mwenye mamlaka katika jamii. Ndoto bado zina nguvu zile zile hata kwa sisi wa leo, hata kama hatuzifatilii kwa kiwango kile kile cha watu wa kale. Ukweli na usahihi wa matokeo ya ndoto huzaa elimu na maarifa ya kila aina.

Ni jambo la kusikitisha sana watu wa leo hawzipi umuhimu mkubwa ndoto, kwa vile hakuwapatikani wafasiri wa kweli wa ndoto.

Mtume Muhammad (saw), mbali ya kuwa Mtume, lakini pia alikuwa kiongozi wa nchi. Kwa sababu hiyo ndiyo maana alipewa na Allah, majukumu mengi na makubwa, kwa ajili ya waumini wake. Alipewa jukumu la kusimamisha **Tauhidi** duniani mahala pa ibada ya masanamu; pia alipewa kazi ya kuwalea kiroho wafuasi wake kwa kuwafundisha ustarabu, upendo, suluhu, utulivu na kudumisha amani na kutafuta elimu ya kumjua Mola wao. Kadhalika alitakiwa kuwahamasisha watu kutafuta maarifa juu ya vitu mbali mbali vya maendeleo na ustawi wa jamii zao. Kwa uzito wa majukumu hayo, inasemekana kuwa, mara zote Mtume (saw) alionekana kuwa mtu wa tafakuri na mtafutaji wa njia za kumuwezesha na kumsaidia kutimiza majukumu yake.

Kwa sababu hiyo Mwenyezi Mungu (SW), kwa fadhila Zake Akamfariji kwa kumuongoza.

Akamtia moyo na kumpa matumaini makubwa ya kushinda katika kila hatua ya juhudi zake. Kwa moyo usiyo choka, Mtume (saw) kwa upande wake aliifanya kazi hii kwa bidii kubwa. Akaijenga jamii mpya ya watu jasiri wapenda Amani, watu wa Tauhidi na wapenda Maendeleo. Jamii hii mpya kwa itikadi yao ya Tauhidi, wakaitwa waislamu na itikadi yao mpya ikaitwa Islamu.

Akiwa katika harakati za kutimiza majukumuyake hayo, Mwenyezi Mungu (sw) Aliwahi mara kadhaa, kuwasiliana na mja huyu kwa njia ya kumpelekea ndoto maalum. Mtume (saw); alipopata ndoto hizo hakukaa nazo kimya, bali alizisimulia kwa watu wake wa karibu. Wale walio bahatika kuzisikia na kuwa na kumbu kumbu nzuri, wali zihifadhi na kuzisimulia kwa watoto wao na jamaa zao. Wengine waliziandika na kuzihifadhi vitabuni. Hatimaye nasi watu wa leo, tumezikuta zimo vitabuni na kupata fursa ya kuzisoma.

### NDOTO ZA MANABII WA ZAMANI

Njia hii ya mawasiliano ghaibu haikuanzia kwa Mtume Muhammad s.a.w, bali ni ya tangu kale; hata manabii wa zamani na wao walipata kuoteshwa ndoto zenye taathira kama za Mtume Muhammad (saw). Qur'an Tukufu, inayo masimulizi mengi ya ndoto za Manabii mbali mbali wa



*Ustadhi A .R. Mikila*

zamani, waliopita kabla ya Mtume Muhammad (saw). Kama vile Nabii Ibrahimu a.s, Nabii Yusufu a.s, na Nabii Musa a.s, na wengingine wengi, wote hao waliwahi kuota ndoto zenye taathira kubwa.

### NDOTO YA NABII IBRAHIMU (A.S)

Nigusie kidogo juu ya ndoto ya Nabii Ibrahimu (as). Nabii huyu mtukufu sana aliwahi kuota ndoto, siku za uhai wake alipokuwa Makka. Ndani ya ndoto ile, alijiona anamchinja mwanae wa pekee na kipenzi chake kuwa sadaka kwa ajili ya Allah, mtoto huyo ni Nabii Ismaili (as). Nabii Ibrahimu alipo amka asubuhi, akaisimulia ndoto hii kwa mwanae na akaitafasiri ndoto hii kwamba, Mwenyezi Mungu (swt) anamtaka kikweli kweli amchinje ili awe sadaka kwa ajili ya Allah. Kwa dhamira na dhana ya kutekeleza amri hii ya Allah, Nabii Ibrahimu alimtaka mwanae kumruhusu atekeleze tendo hilo. Nabii Ismaili a.s, alimruhusu baba yake, na akasema: " utanikuta Inshaallah miongoni mwa wanao subiri".

Qur'an Tukufu, inasema:-

"Basi alipofika umri wa kuweza kukimbia na kutembea naye, (Ibrahihimu ) akasema: Ewe mwanangu, hakika nimeona katika ndoto nina kuchinja, basi fikiri waonaje? (Mtoto) Akasema: Ewe baba yangu fanya unalo amriwa, utanikuta Inshaallah miongoni mwa wanao subiri. Basi wote wawili walipo ridhia na akamlaza kifudifudi. Mara Tukamwita: Ewe Ibrahimu, Umekwisha isadikisha ndoto. Kwa yakini hivi ndivyoTuwalipavyo watendao wema. Bila shaka hili ni jaribio bayana. NaTukamkomboa kwa dhabihu kubwa. Na Tukamwachia sifa kwa watu wa baadaye. Amani iwe kwa Ibrahimu" (Qur, 37:103- 110).

Ndoto hii ni maarufu sana kwa waislamu, kwa wayahudi na hata kwa wakristo. Hakuna kundi hata moja linalo kanusha ukweli wa ndoto hii. Bali ipo dhana kwa upande wa wayahudi kwamba, mwana wa sadaka aliye kusudiwa hapa, alikuwa ni Nabii Is-haka na siyo Nabii Ismaili. Dhana hiyo haiondowi au kukanusha ukweli kwamba, Nabii Ibrahimu aliota ndoto na katika ndoto ile alijiona anamchinja mwanae wa pekee.

**Nini kilitokea baada ya ndoto hii?**

Ndoto hii ilileta matokeo makubwa na ya ajabu sana!

Muda mchache tu kupita baada ya ndoto hii, Nabii Ibrahimu alianza kazi ya kujenga Kaaba, nyumba ya ibada ya Mungu mmoja. Kwa mara ya kwanza dunia ikapata nyumba ya kumuabudia Allah na ikawa ndiyo kumbu kumbu ya dhabihu hii kubwa hadi leo. Pia dunia ilipatiwa kituo cha kwanza cha Hija.

Qur'an Tukufu inasema:-

"Na (kumbukeni) Ibrahimu alipoiinua misingi ya Nyumba, na Ismaili (wakaomba): Mola wetu Utupokelee *maombi yetu*, hakika Wewe ndiye Mwenye kusikia Mwenye kujua" (2:128)

Kituo hiki cha hija kilipatikana baada ya dhabihu hii kubwa. Hija tangu kale hufanyika Makka kwa nabii Ismail (as), siyo Jerusalemu kwa nabii Is'haka. Zile pilika pilika za Mahaji kule Makka; yaani kutufu Kaaba, kumpiga mawe shetani, kunyoa nywele na kuchinja wanyama kwa maelfu; kwenda Arafa, kwenda Muzidalifa na Minna. Shughuli zote hizo na nyinginezo, ni kumbu kumbu ya tukio la ndoto ile ya kuchinja ya Mchamungu huyu na mwanae Ismaili a.s. Wakazi wa Makka na vitongoji vyake, wanalo deni kubwa la kulipa la dhabihu hii. Kwa sababu tangu siku ile ilipo tolewa dhabihu hii kuu, hadi leo wao wana faidi na kunufaika na matunda mazuri yanayo patikana kutoka katika ndoto hii.

### NDOTO YA NABII YUSUFU (AS)

Nabii Yusufu a.s, mtoto wa Nabii Yakubu (as), mjukuu wa Nabii Ibrahimu (as) aliwahi kuota ndoto akiwa bado yungali mdogo kabisa, wakati ndugu zake walipo panga kumuuwa kwa husuda. Ndoto yake hii, imetajwa ndani ya Qur'an tukufu katika Sura Yusufu (12) aya ya 5-6.

Katika ndoto, nabii Yusufu (as) aliona onyesho kuu. Alililona Jua, Mwezi na Nyota kumi na moja vyote vikimsujudia.

"(Kumbuka) Yusufu alipo mwambia baba yake: Ewe baba yangu, hakika mimi nimeona (katika ndoto), nyota kumi na moja na jua na mwezi nimeviona vikinisujudia. (Baba yake) Akasema: Ewe mwanangu usisimulie ndoto yako kwa ndugu zako, wasije wakakufanyia hila. Hakika shetani kwa mwanadamu ni adui dhahiri" (Kur 12:5-6).

Wana historia na wasomaji wa Biblia, wanaifahamu vizuri ndoto hii. Wanaitaja kwa utukufu mno na kusema kuwa, ndoto hii ndiyo iliyozaa safari ya uhamisho wa Wana Israel kutoka Kanani kwenda kuishi Misri. Na baada ya muda mrefu wa ustawi wao kule Misri, mambo yaliwageuka walitoka kwenye raha wakaingia kwenye mateso makubwa na ya miaka mingi, chini ya utawala wa Firauni (Farao).

### NDOTO YA NABII MUSA (AS)

Kadhalika ipo ndotoya Nabii Musa (as), inayo simuliwa na Qur'an Tukufu.

Nabii Musa (as) aliwahi kupata **kashfi (**ndoto bila kulala**)**, alipokuwa anasafiri na ahali zake kuelekea Misri akitokea Midiana kwa mkwewe Nabii Shuwaibu (as). Akiwa njiani, kwa mbali akauona moto maalum unawaka. Hapo akawaambia ahali zake nisubirini niende kwenye moto ule, huenda nikawaletea habari za huko au kijinga mwote.

Qur'an tukufu inasema:-

"Basi Musa alipo timiza muda, akasafiri pamoja na ahali zake. Akaona moto upande wa mlima. Akawaambia ahali zake. Ngojeni hakika nimeona moto labda nitawaleteeni habari za huko au kijinga cha moto mwote. Basi alipo ufikia aliitwa kutoka upande wa bonde katika kiwanja kilicho barikiwa kutoka mtini ya kwamba ewe Musa, bila shaka Mimi Ndiye Allah Mola wa ulimwengu. Na ya kwamba tupa fimbo yako. Basi alipo iona ikichezacheza kama nyoka akageuka (kukimbia) bila kutizama nyuma. Ewe Musa, njoo mbele usiogope, kwa yakini wewe u miongoni mwa walio salimika"(Kur 28:30-32).

Inafahamika kwa mapana makubwa kwamba, ndoto hii ndiyo iliyozaa vugu vugu la ukombozi wa wana Israeli. Nabii Musa (as) ailiingia Misri kwenda kuwakomboa Wana wa Israeli na kuwapeleka Kanani. Alipofika Misri Nabii Musa a.s, alianzisha harakati za kudai uhuru wa wana Israeli kwa Firauni (Farao). Hatimaye alifanikiwa kuwatoa wana wa Israeli katika makucha ya mfalme Yule katili, na kwenda nao kanani. Akiwa njiani alipitia tena katika milima ya Sinai. Katika mara hii ya pili, nabii Musa (as) alipokea ufunuo na Amri 10 za Mungu- yaani Taurati. Haya ndiyo matokeo ya ndoto hii ya kuona moto. Moto ulitabiri ushindi kwa Nabii Musa(as) wa kuwatoa Wana wa Israeli utumwani na kuwapa uhuru.

Leo hali ya mafanikio ya Wayahudi ipo wazi na inatisha! Wayahudi wapo juu sana leo, wamekuwa wababe, wapenda vita na utawala. Taifa lao lina nguvu kubwa za kijeshi na maarifa mengi ya vita, waarabu wa nchi zote za ukanda wake, wapo hoi wamekuwa wanyonge.

***Inaendelea toleo lijalo, Inshallah***

# Shujaa wa ukombozi wa Tanzania

**Na Mahmood Hamsin Mubiruu**

Tanzania ingelikuwa na utamaduni wa kuhifadhi na kuheshimu kumbukumbu za historia yake, hapana shaka kifo cha Sheikh AbdulKarim Sharma kingelikuwa ni msiba mkubwa wa taifa, kwani mchango wake kwa ukombozi wa nchi hii ni mkubwa na kwa wale wanaojua 'Inshallah' siku moja itakapoandikwa historia na watu wenye uadilifu Sheikh Abdulkarim Sharma atapewa nafasi yake anayostahili. Kwani ni Sheikh AbdulKarim Sharma aliyefanya shughuli za Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika jiji la New York kuwa rahisi kidogo kwa sababu alimpatia barua ya utambulisho ya kwenda kwa Sir Muhammad Zafrullah Khan ambaye toka mwaka 1947 alikuwa Waziri wa nchi za nje wa taifa jipya la Pakistan. Wakili huyu maarufu alimsaidia sana Mwalimu Julius Nyerere katika kuwakilisha hoja yake katika baraza la udhamini la umoja wa Mataifa. Haukuwa mchango mdogo hata kidogo. Kwa majonzi makubwa tumepokea habari za kifo chake na lolote lile hatuna, ila kauli yetu ni *'Innalillahi wa inna ilaihi raajiun'*. Sisi ni wa Mwenyezi Mungu na Kwake tutarejea.

Sheikh AbdulKarim Sharma ambaye baba yake alikuwa Sahaba wa Masihi Aliyeahidiwa- Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as) alizaliwa tarehe 26 Mei, 1908 siku ile ile alipofariki Masihi Aliyeahidiwa (as). Mwaka 1939 alifaulu mtihani wa Moulvi Fazal katika chuo kikuu cha Punjub na mwaka 1941 alimaliza darasa la 10. Mara baada ya tangazo la Kalifa Mtukufu wa Pili - Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad kutangaza watu kujitolea katika dini ya Islam Sheikh AbdulKarim Sharma alikuwa miongoni mwa watu wa mwanzo kujiunga na jeshi hilo. Akiwa pamoja na Maulana Sheikh Muhammad Munawwar walikwenda kumuwaga Khalifa wa Pili ambaye aliwaombea maombi marefu sana ili wapate mafanikio katika kazi zao na hatimaye kuwakumbatia, Sheikh Sharma alieleza baadaye kwamba hiyo ni siku ya pekee katika maisha yake ambayo hakuisahau. Tukio hili ni muhimu sana kwani linadhihirisha dhahiri ni jinsi gani Khalifa Mtukufu wa Mwenyezi Mungu maombi yake yanavyokubaliwa. Na ni kweli kabisa ya kwamba kazi aliyoifanya Sheikh AbdulKarim Sharma na Sheikh Muhammad Munawwar ni kazi zilizo tukuka na ni kazi za kupigiwa mfano.

Tarehe Mosi Januari, 1945 mwishoni mwishoni mwa



*Maulana Sheikh AbdulKarim Sharma*

vita ya pili ya dunia, Sheikh AbdulKarim Sharma na Sheikh Muhammad Munawwar waliingia katika meli ya SS - KARANJA na kuwasili Afrika Mashariki mwaka 1948. Sheikh Muhammad Munawwar alishuka katika jiji la kale la Mombasa na Sheikh AbdulKarim Sharma akaingia jiji la Dar es salaam tarehe 05, August, 1948. Kuwaona tu Waafrika alikwenda pembeni mwa meli hiyo na kufanya maombi marefu yaliyoambatana na kwikwi na vilio. Huku akilia aliomba; "Ee Mola Umenijaalia kufika katika Ardhi hii, nipe uwezo, nguvu, na hekima ya kuwatumikia viumbe wako. Nijazie mapenzi moyoni kwa ajili yao ili niweze kuwatumikia". Dua hii ilikubaliwa kwani aliyowafanyia Waafrika ni vigumu kuyasahau. Baada ya kupita Arusha, Machame, Lushoto, Tabora, Moshi akihubiri mwisho aliletwa tena Dar es salaam.

Lakini kabla hatujaona yote yaliyofanyika, hebu tutazame angalau kwa akali jinsi gani dua yake ya kuwapenda Waafrika na kuwatumikia ilivyokubaliwa.

Katika safari zake za Mahubiri Sheikh AbdulKarim Sharma huku akichanganyika na wenyeji, akila chakula wanachokula, alifika Arusha na sehemu nyingi za Moshi mkoani Kilimanjaro ambako alihubiri na kufungua matawi ya Jamaat. Kabla ya siku si nyingi tayari alikuwa amepata maneno mawili - matatu ya kichaga. Jamaat ya Machame kwa kiwango kikubwa maendeleo yake yananathibishwa na Sheikh AbdulKarim Sharma. Ni katika Jamaat hii ndipo tumepata Wabashiri maarufu wa Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya. Mwalimu Shaaban Shoo ambaye alikuwa ni Mwalimu wa Jumuiyya na Mbashiri wa kujitegemea kwa miaka mingi amefanya kazi ya sifa na ya kuheshimiwa huko Machame na sehemu nyingine nyingi hapa nchini. Mwalimu Abdul Imran Mganda ambaye amefanya kazi kubwa sana ya Mahubiri naye ni mwenyeji wa sehemu hiyo ya Machame.

Akiwa huko Moshi, Sheikh AbdulKarim Sharma alitembelea sehemu nyingi na alikwenda kumuona Chifu wa Wachaga Augustus Mareale. Kutokananamahubiriyahekima na busara urafiki mkubwa ulifungika baina ya Sheikh na Chifu. Ulikuwa ni urafiki wa mapenzi na kuheshimiana. Miaka mingi baadae waliendelea kuandikiana na Sheikh AbdulKarim Sharma alikumbuka ukarimu wa Chifu na mkewe ambaye alijitahidi sana kumpikia chakula cha kwao yaani chapati. Ni masikitiko makubwa kwamba hivi leo Waislam na Wakristo eti hawawezi kuwa katika chombo kimoja, na eti patachimbika. Mfano ni huo kutoka kwa Sheikh AbdulKarim Sharma na Mwaminio siku zote huokota hekima popote anapoikuta.

Sheikh AbdulKarim Sharma pia alifunga urafiki mkubwa na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Mwaka 1954 chama cha TANU kilipozaliwa, Mbashiri Mkuu wa Jamaat Ahmadiyya hapa nchini alikuwa Sheikh AbdulKarim Sharma. Upo ushahidi wa kutosha kwamba barua nyingi za TANU zilizokuwa zinaandikwa kwa matawi mengi nchini zilichapiwa Ofisini kwa Sheikh AbdulKarim Sharma na mara kwa mara viongozi hawa waliweza kualikana kwenye chakula. Sheikh Sharma pia aliwahi kufunga safari ya kwenda Unguja na huko alikuta uhasama mkubwa uliotokana na ubaguzi wa rangi na akapata fursa ya kuzungumza na viongozi wa kambi mbili akiwakumbusha kwamba wote ni binadamu walio sawa na ubora wa mtu hautokani na rangi yake, bali ni khulka na mwenendo wake. Mawaidha haya ya Sheikh AbdulKarim Sharma ndiyo yaliyofanya vyama vya kisiasa huko Unguja kuanza kushirikiana na hatimaye mwaka 1964 tarehe 12 Januari yalitokea mapinduzi ambayo kwa kiwango kikubwa yalishirikisha vyama vingi vya kisiasa vya visiwani humo.

Tukiendelea na maudhui ya dua yake ya kumuomba Mwenyezi Mungu Ajaze mapenzi ya watu wa nchi hii kwake. Mapenzi aliyoyajenga Sheikh AbdulKarim Sharma miongoni mwa Wanajumuiyya yalikuwa makubwa kiasi hiki ya kwamba Bi. Radhia Kaluta Amri Abedi alipotaka kuolewa na Bwana Mbululo, Bi. Radhia alimwambia aende kuomba idhini kutoka kwa Sheikh AbdulKarim Sharma ambaye alimuhesabu kuwa baba yake hiyo ni dalili kubwa ya mapenzi na heshima.

Masheikh hao wawili waliotoka wote Pakistani kuja Afrika Mashariki Sheikh AbdulKarim Sharma na Sheikh Muhammad Munawwar walionesha mapenzi makubwa kwa wananchi na sehemu hizi za Afrika. Nakumbuka mwaka 1982 katika hotuba moja ya Ijumaa Sheikh Muhammad Munawwar alisema; "Nikifa nizikwe pamoja na ndugu yangu pale Temeke". Tazama mapenzi waliyokuwa nayo Masheikh hawa wawili walionesha mapenzi aliyoyasema Masihi Aliyeahidiwa (as) ya udugu wa dhati.

Mchango wa Sheikh AbdulKarim Sharma kwa maendeleo ya Jumuiyya ulikuwa mkubwa. Ndiye aliyepigania tupate kiwanja cha makaburi kilichopo Temeke. Huko nyuma ilizuka fitina. Kaburi la mtoto wa Nazir Ahmad Dar liliharibiwa. Ili kuondoa fitina hiyo ndipo Sheikh AbdulKarim Sharma alipoingia katika harakati za kupata mahali pa makaburi kwa ajili ya Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya. Ni yeye pia aliyekamilisha michoro ya makaburi hayo inayoonesha mahala pa kuoshea maiti na mahali pa kutawadhia.

Itakumbukwa kuwa gazeti la Mapenzi ya Mungu lilisajiriwa mara ya pili Nairobi - Kenya. Kuna kipindi palikuwepo na mgogoro baina ya Kenya na Tanzania, hivyo Sheikh AbdulKarim Sharma alionelea ni vyema kulisajili gazeti hili tena mara ya tatu hapa Tanzania mwaka 1973.

Msikiti wa Masjid Salaam uliyoko hapa Dar es salaam ulisimamiwa ujenzi wake toka mwanzo hadi mwisho na Sheikh Abdulkarim Sharma. Naye ndiye aliyehusika katika ufunguzi wake mwaka 1957.

Tukio la kihistoria ambalo Sheikh Abdulkarim Sharma analikumbuka sana ni pale alipopambana na mhubiri wa Kikristo Dr. Rush. Msomi huyo wa Kikristo alikuwa na uwezo mkubwa wa kujieleza na mihadhara yake ilivuta watu wengi. Licha ya uwezo wake huo wa kuhubiri alikuwa ameandika kitabu alichokipa jina '*Jinsi dini ya Islam ilivyotungawa*'. Kwa sauti ya upole na heshima Sheikh Abdulkarim Sharma alimwambia Dr. Rush kuwa haikuwa makamu yake kuandika kitabu kama kile. Alichotakiwa ni kuchukua tambio la kuandika kitabu kama Qur'an Tukufu, jambo ambalo wameambiwa hawawezi. Mtaalamu huyo alibaki kinywa wazi na wala hakudiriki kujibu hoja hiyo. Katika masuala ya dini Sheikh Abdulkarim Sharma alikuwa imara sana. Huko Tabora kulikuwa na tafrija ya kumkaribisha Gavana Edward Twining. Watu wote walipeana mikono na mke wa Gavana, yeye alipofika kwa mke wa Gavana akwambia ya kwamba sawa na mafundisho ya Islam wanawake hawapeani mikono na wanaume. Wakati wa vinywaji na chakula Gavana mwenyewe alimwambia mhudumu; 'weka mbali pombe hiyo hapo kuna Sheikh'.

Sheikh Abdulkarim Sharma atakumbukwa sana Afrika Mashariki kwa mchango wake mkubwa wa kuleta nuru wakati wa giza, na atakumbukwa sana kwa kusaidia kuleta uhuru wa nchi hii kwani hakuna taifa lolote linaloweza kupata maendeleo kama limegubikwa na giza la ukoloni.

Kutawaliwa labibu,
mtu hakui upesi
Yako mema maarubu,
hayaachiwi nafasi
Watapenda uwe bubu,
wa kunyonye kipapasi
Uhuru jambo halisi,
kuukosa ni taabu

# Bustani ya Washairi

**WASIOJUA MIZUNGU HAO NDIO TUWAZOME**

1 Bismillahi ni mwanga, wa kila kazi ya mtu
Unaepusha majanga, ni dawa ya utukutu
Na wajuao ni kinga, kwa yale si hasanatu
Wasiojua mizungu, hao ndio tuwazome

2 Ewe Kungwi bin Mbanga, nipo sijaenda kwetu
Kimbangulile hajenga, ndiko maskani kwetu
Sijaondoka malenga, ningekwambia manitu
Wasiojua mizungu, hao ndio tuwazome

3 Huwo witowo wakunga, ulotolea sautu
Ya kuniita nyikanga, weye nami tusukutu
Kumekuja damu changa, waifuje fani yetu
Wasiojua mizungu, hao ndio tuwazome

4 Wawili tutajipanga, nani atayethubutu
Wengine wakijiunga, si vibaya ni wenzetu
Ole watia mchanga, Kiswahili lugha yetu
Wasiojua mizungu, hao ndio tuwazome

5 Wawapi hao kiranga, wapo kwenye mafukutu?
Wapi walikojipanga, katika huo msitu?
Wako hapa au Tanga, nieleze mwanakwetu
Wasiojua mizungu, hao ndio tuwazome

6 Rudisha kwanza mizinga, bomu na roketi zetu
Nguvu nyingi umelenga, mkubwa uwezo wetu
Isije tukawanyonga, hata maswahiba zetu
Wasiojua mizungu, hao ndio tuwazome

7 Hao wanaobananga, tufanye doria yetu
Tuone wana mianga, humu mwenye fani yetu
Penginewe ni ujinga, tulete darasa letu
Wasiojua mizungu, hao ndio tuwazome

8 Utume jeshi la anga, lenye taaluma yetu
Walojitoa muhanga, wawili ama watatu
Wakapelekeze kugna, jilopigiwa upatu
Wasiojua mizungu, hao ndio tuwazome

9 Hakika ikitujenga, hisia ya nyoyo zetu
Ikidhihiri tasonga, kwa kitali kati yetu
La kufanya kuwagonga, wakome kwa utukutu
Wasiojua mizungu, hao ndio tuwazome

10 Tukiona wanapanga, mikuki na kila kitu
Jambia sime na donga, tayari kuuwa watu
Tutasogeza mizinga, ile nyuklia yetu

Wasiojua mizungu, hao ndio tuwazome

11 Nakuhakikia Mbanga, madamu tuhai watu
Kwa fasaha tutabonga, hiki Kiswahili chetu
Ajaye kwa kutobanga, ajuwe halali yetu
Wasiojua mizungu, hao ndio tuwazome

12 Tuwazome kwa kuwinga, wende papatupapatu
Wende wakitangatanga, sisi tuwe wa kufutu
Kwenye titimanga, wawe wa magutugutu
Wasiojua mizungu, hao ndio tuwazome

13 Wassalaamu tutachunga, tutahami lugha yetu
Kwa tungo njema kutugna, zilosheheni ladhatu
Zenye rojo za kukonga, ziso kauka kukutu
Wasiojua mizungu, hao ndio tuwazome

***Al-Ustadh Khamisi Sultani Wamwera***
***Mbagara Kimbangulile Rangi tatu - Dar es salaam.***

**ONGEZA ZANA VITANI**

1. Labeka thumma labeka, kungwi mwanawe Mmbanga
Mawazo yamenyooka, utadhania upanga
Rabbi Akupe baraka, uzidi lugha kujenga,
Ongeza zana vitani, tuyalinde mashairi

2. Umeita naitika, tungo wanaziboronga
Hawamaizi mipaka, beti wanazitobanga
Shufu zilivyopauka, mithili jora la kanga
Ongeza zana vitani, tuyalinde mashairi

3. Ni lipi la kufanyika, kutibu wenye kilanga
Kwanza dua kwa Rabuka, wamanye nao kutunga
Kipaji huteremka, toka Muumba wa anga
Ongeza zana vitani, tuyalinde mashairi

4. Pili wanawajibika, kuwadurusu nyakanga
Wa Robati msifika, mahiri Mmanyakunga
Na Kaluta kadhalika, wasome alivyotunga
Ongeza zana vitani, tuyalinde mashairi

5. Qaditama nimefika, usemi wangu nafunga
Katufunza mwana Makka, maneno mengi si mwanga
Yakikitihiri dhihaka, hatimaye ni kuvunga.
Ongeza zana vitani, tuyalinde mashairi

***Mahmood Hamsin Mubiru (Wamamba)***

**CHAI**

1. Kwa jina lake Qudusi, nataka kuhutubia
Wala sifanyi kisasi, chai kuishambulia
Ila kwa kadamnasi, msisitizo natia
Chai kinywaji udhia, japo hudara mitima

2. Wengi hupita kiasi, chai wakiisifia,
Kila wakati kuhisi, ni muda wa kujinywia,
Huu ni muono hasi, si wa kuung'ang'ania
Chai kinywaji udhia, japo hudara mitima

3. Ni kinywaji mahususi, chai katika dunia
Ni sharubati nyepesi, kooni hujishukia,
Lakini ina utesi, wanywao hugugumia,
Chai kinywaji udhia, japo hudara mitima

4. Hudhani tiba rahisi, chai wanaotumia,
Kwa kuponya uyabisi, tumboni uloingia,
Wakaipa na makisi, ya matunda asilia
Chai kinywaji udhia, japo hudara mitima

5. Wajuao ufanisi, chai wanatuambia,
Kileo cha wafuasi, wanaoikimbialia,
Iwe chungu na kakasi, hunywa wakivulimia
Chai kinywaji udhia, japo hudara mitima

6. Hushikwa zao nafusi, chai wanofakamia,
Wakadhani ni fususi, ya bei kugharimia,
Bali wenye faharisi, si hasha huikimbia,
Chai kinywaji udhia, japo hudara mitima

7. Ina mwingi utatasi, chai ukiipapia,
Tena ina ubilisi, ukiisikilizia,
Na ukiipa nafasi, hadhi hukuchafulia,
Chai kinywaji udhia, japo hudara mitima

8. Sinuwii kuitusi, chai kuiharibia,
Ila nimetahasusi, siri kuwafichulia,
Mwaweza kufa upesi, mkinywa kwa kupania,
Chai kinywaji udhia, japo hudara mitima

9. Ni ukweli si tetesi, chai inawaghumia,
Daima huwapa kesi, wanaoishabikia,
Na hata kuwafilisi, wanoihangaikia,
Chai kinywaji udhia, japo hudara mitima

10. Chonde msije nighasi, sijawaharamishia,
Ni halai siisusi, ingawa naichukia,
Nitainywa kwa kiasi, haja ikinizidia
Chai kinywaji udhia, japo hudara mitima

***Abdullah Hamisi Mbanga (Kungwi)***
***Tambani - Mkurungana Pwani***

**KITI**

1. Lazima utaondoka, kiti ulichokalia
Usambe ni patashika, mipango yake jalia
Mpandangazi hushuka, ndio mwendo wa dunia
Kumbuka usisahau, mpandangazi hushuka

2. Kiti hicho walishika, na kikubwa kuzidia
Hawakuzua shabuka, wala kujitutumua
Walimuhofu Rabuka, Alotuumba insia
Kumbuka usisahau, mpandangazi hushuka

3. Ukikaa nakumbuka, wapo walotangulia
Sasa wameshatoweka, kwenye shimo liso taa
Mola Ameshawashika, wapi watakimbilia
Kumbuka usisahau, mpandangazi hushuka

4. Hivyo kiumbe geuka, uache kujifutua
Kumbuka ulikotoka, na wapi waelekea
Cheo ulevi hakika, siri ninakumegea
Kumbuka usisahau, mpandangazi hushuka

5. Elewa utazimika, huo wako mshumaa
Hata kama unawaka, na nuru kuangazia
Ipo siku itafika, upepo utapepea
Kumbuka usisahau, mpandangazi hushuka

6. Kaditama nimefika, kituoni ninatua
Nakuomba kuliweka, pia kulizingatia
Ni wazo lenye baraka, kumulika yako njia
Kumbuka usisahau, mpandangazi hushuka.

***Na Mahmood Hamsin Muburu (Wamamba)***
***Dar es Salaam***

**SIFA ZARUDISHWA KWAKE**

1 Sifa zarudishwa kwake, Mola wetu Msifika
Sisi wote waja wake, hakuna alotukuka
Bure heshima utake, takufa kifo cha nyoka
Kamwe siiachi haki, mimi ni Ahmadiyya

2 Kamwe sitishiwi nyau, kama mtoto mdogo
Ni mkubwa angalau, katu sirambwi kisogo
Vije vita mau mau, na wenye hasira mbogo
Kamwe siiachi haki, mimi ni Ahmadiyya

3 Sulemani mwana kingo, nimefika mwisho wangu
Nimeshakuta ukingo, wa ile safari yangu
Hapa nimeramba bingo, sitoki nyie wenzangu
Kamwe siiachi haki, mimi ni Ahmadiyya

4 Mje na jua kulia, na vito vyenye thamani
Nyota nao mwezi pia, mvishike mkononi
Vyote nitavitakimbia, nitakwenda kwa Manani
Kamwe siiachi haki, mimi ni Ahmadiyya

5 Muwe na mingi mikuki, na silaha nzito nzito
Mtege na mafataki, katu siitiki wito
Mniwekee bunduki, sijali wake mkito
Kamwe siiachi haki, mimi ni Ahmadiyya

6 Niueni mfaidi, nyoyo zenu kuzipoza
Nitakufa kishahidi, kama cha Bwana Hamza
Kulikoni kuritadi, nikamuudhi Aziza
Kamwe siiachi haki, mimi ni Ahmadiyya

7 Daima tasonga mbele, maadamu nipo hai
Nyie bakini milele ,Toeni wangu uhai
Na mpige makelele,sibadili yangu rai
Kamwe siiahi haki, mimi ni Ahmadiyya

8 Mtangaze kila kona,kwamba mimi ni kafiri
Wala Suni sitaona Isa hajafa sikiri
Nitang'ang'ania sana,kwamba yu kwenye kaburi
Kamwe siiachi haki, mimi ni Ahmadiyya

9 Tukaneni waziwazi, nitaziba masikio
Katu Mola simkwazi, sitawajibuni ndio
Nitasimama pa wazi, kupinga ya kifarao
Kamwe siiachi haki, mimi ni Ahmadiyya

10 Masih kanifikia, ninaemwangu moyoni
Siwezi kuwazuia, wakwenu msubirini
Katu hatawashukia, milele mngojeeni
Kamwe siiachi haki, mimi ni Ahmadiyya

11 Vyeo hajajipandisha Masih wake wadudi
Tena hajatufundisha tumkane Muhammadi
Amekuja kurudisha Masheikh waloritadi
Kamwe siiachi haki, mimi ni Ahmadiyya

12 Asuuhi Ishafika,kumeshakucha kweupe
Funuweni zenu shuka, muangaze zenu kope
Acheni kushikashika, lama ya mdudu kupe
Kamwe siiachi haki, mimi ni Ahmadiyya

13 Nakuomba nihifadhi, Moka wangu Mtukufu
Niepushe na maradhi, ya Ghafaru ya Raufu
Tene uniwie radhi, yote yangu mapungufu
Kamwe siiachi haki, mimi ni Ahmadiyya

14 Rabi unijaalie, nife ni Muislamu
Fungu langu nitunzie, niepushe na haramu
Dua nitakabalie, niweke kwenye nidhamu
Kamwe siiachi haki, mimi ni Ahmadiyya

***Suleimani Kingo***
***Masomoni - Uganda.***

**HONDO HONDO KAUMIA**

1 Maporini kuna ndege, Hondohondo jina lake
Si mdogo kama nzige, mkubwa umbile lake
Humuwezi umfuge, hasa kwa tabia yake
Hondohondo kaumia, kaponzwa na wema wake

2 Yeye hutaga mayai, katika kiota chake
Kutwa kutwa hatembei, anashinda peke yake
Hukataa maadui, wasile mayai yake
Hondohondo kaumia, kaponzwa na wema wake

3 Na hata akitotoa, huzidisha wema wake
Hata mbawa huzing'oa makusudi asiruke
Shariti atapokua, sawa na makinda yake
Hondohondo kaumia, kaponzwa na wema wake

4 Mzingwi na Tongwanyundo, walimuendea kwake
Kumwambia hondohondo, apunguze wema wake
Utamletea ng'ondo, katika maisha yake
Hondohondo kaumia, kaponzwa na wema wake

5 Lakini alikaidi, rai ya ndege wenzake
Kajing'oa makusudi, makinda yale si yake
Wenyewe waliporudi, zikaanza pekepeke
Hondohondo kaumia, kaponzwa na wema wake

6 Ndipo walipogombana, na wengine wamshike
Awaeleze bayana, sababu na chanzo chake
Yeye la kusema hana, huo ndio wema wake
Hondohondo kaumia, kaponzwa na wema wake

7 Ndipo likazuka zogo, majogoo na majike
Kanasa kwenye mtego, kakung'utwa kwa mateke
Kaumizwa kwa kipigo, kalala asiinuke
Hondohondo kaumia, kaponzwa na wema wake

8 Vikatokea vituko, kwa wale jirani zake
Vya nderemo na vicheko, ndipo watu wasituke
Wamuweka kitako, imekwisha kazi yake
Hondohondo kaumia, kaponzwa na wema wake

9 Wenzie walimkanya, na yeye asikumbuke
Kaongeza kukusanya, na mayai ya wenzake
Eti alijidanganya, awe mwema peke yake
Hondohondo kaumia, kaponzwa na wema wake

***Sihiyana Swalehe Mandevu (Mtendamema)***

# Kutoka Dar hadi Bukoba

Na Mahmood Hamsin Mubiru

Safari yangu kutoka Dar es salaam hadi Bukoba ilifanikiwa kuuwa ndege wawili kwa jiwe moja. Nilipata heshima ambayo labda sisitahili ya kuwakilisha Jumuiyya ya Ahmadiyya katika kongamano la kimataifa lililokutana ili kukumbuka nusu karne toka atawafu Shaha wa malenga Shaaban Suleiman Ufukwe maarufu Shaaban Robert. Ndege wa pili nilifanikiwa kumpata kwa kuwaona ndugu zangu wa damu na wa kiroho na kukanyaga ardhi ambayo imetunza kitovu changu.

Safari hii ina historia. Mwaka 1959 katika ukumbi wa mikutano na maktaba msikiti wa Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya - Dar es salaam ulifanyika mkutano wa kwanza wa washairi wote nchini. Mwenyeji wa mkutano huo alikuwa Sheikh Kaluta Amri Abedi. Kwa kukumbuka mchango huo baraza la taifa la Kiswahili bilhususi Mwenyekiti wa UKUTA mkoani Kagera Bwana Abdallah Msakanjia wa Ndoto tamu Katoro alifika makao makuu ya Jumuiyya ya Ahmadiya na kutoa mwaliko kwa Jumuiyya ya Ahmadiyya kuhudhuria kongamano hilo



*Bwana Abdallah Msakanjia Mwenyekiti wa UKUTA Kagera*

na kuwasilisha mada. Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya Tanzania Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry alipokea mwaliko huo kwa mikono miwili na akaniteua niwakilishe Jamaat katika kongamano hilo na nikapewa fursa ya kutoa mada. Nilitayarisha mada yenye anuawani '*Usuhuba wa Shaabani Robert na washairi wenzie*'.

Bwana Amir Abedi Kaluta ambaye anaheshimika kutokana na harakati za kukuza Kiswahili ambazo zilidhihirika wakati wa uzinduzi wa kitabu cha baba yake kilichoandikwa na Bwana Mathias Mnyampala '*Historia ya maisha ya Sheikh Kaluta Amri Abedi*'. Kutokana na harakati hizo, Bwana Amir Abedi alipewa mwaliko na mratibu wa kongamano hilo Bw. Abdallah Msakanjia. Yeye alitangulia na mimi nilikuja siku moja baadaye. Kwa msaada wa Mwenyezi Mungu alibeba vitabu vya Jumuiyya na gazeti la *Mapenzi ya Mungu* ambalo lilikuwa ni toleo maalum la kumbukumbu ya Shaaban Robert kutimiza nusu karne tangu amefariki.

Shukrani zote ni kwa Mwenyezi Mungu Aliyenijaalia na kunirahisishia safari hii. Na katu huwezi kumshukuru Mwenyezi Mungu kama huwashukuru binadamu. Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry ana mchango mkubwa katika kufanikisha safari hii. Mwalimu Mkuu msaidizi wa shule ya Alpha High School Bw. Jovitha alikuwa na karata ya turufu na Mkuu wa taaluma Alpha High School Bw. Vitalis aliondoa giza lililokuwa limetanda kwa kutamka neno moja tu 'nenda'. Niliondoka Dar es salaam asubuhi ya Jumatatu ya tarehe 19 Agost, 2013 na kuwasili mjini Bukoba siku ya Jumanne tarehe 20 Agost, 2013. Nilipokelewa kwa heshima zote na Bw. Magera Nsubuga Mkurugenzi wa kampuni ya Fair Play, mara nilimpa taarifa ya kufika kwangu Bw. Msakanjia ambaye hakufanya ajizi bali alikuja na gari lake hadi ukumbi wa mkutano wa Mtakatifu Francis ulioko karibu na shule ya Rumuli. Nnilitambulishwa kwa wana kongamano ambao walikuwa wamefurika kwenye ukumbi huo. Wana kongamano hao walikuwa wametoka Kenya, Uganda, Ghana na wasomi maarufu wa Kiswahili Profesa Mulokozi na Profesa Rubanza. Wana kongamano hao walitoa wito wa kuendelea kuwaenzi wale waliyoitumikia kwa moyo mmoja Lugha ya Kiswahili. Mapenzi ya Kiswahili mashuleni ni jambo lililosisitizwa sana, kwani ni walimu ndio wanaoweza kujenga mapenzi ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi. Ulitolewa mfano wa Mwalimu Kiimbila ambaye alitoa mchango mkubwa katika kustawisha Kiswahili shule ya Nyakato na Tanzania kwa ujumla. Kongamano lilikubaliana kuzuru kabuli la Mwalimu Kiimbila ikiwa ni alama ya kuheshimu mchango wa Mwalimu huyo.

Kongamano hilo litoa mwito wa kukusanya maandiko ya washairi ili yaweze kuchapwa. Kongamano lilieleza juu ya mashairi ambayo tayari yemekwisha kusanywa yakiwemo ya Bw. Shaabani Chuma Gonga, Bw. Mohamed Alli na Sihiyana Salehe Mandevu (Mtendamema). Mchakato umo mbioni wa kuchapisha diwani hizo.

Kongamano pia lilitoa shukrani za pekee kwa Mwenyekiti wa UKUTA Kagera Al-Ustadh Abdallah Msakanjia na Profesa Mulokozi ambao hawakupata lepe la usingizi kwa ajili ya kuhakikisha kufanikiwa kwa kongamano hilo. Kongamano kwa sauti moja liliwapa shumbe - hongera watetezi hao wakubwa wa lugha ya Kiswahili.

# Safari ya kihistoria mkoani Kagera

**Na Mwandishi wetu**

Tanzimu ya Lajna Imaillah ambayo ni taasisi ya akina mama wa Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya ina mpango kabambe na endelevu wa kutembelea matawi yake ambayo yametapakaa nchini kote.

Katika kutimiza adhma hiyo, Rais wa Tanzim hiyo ya Lajna Imaillah Tanzania - Mwanasheria Bi. Muamini Kazema alifanya ziara ya kutembelea matawi ya taasisi hiyo yaliyopo mkoani Kagera. Sawa na historia hiyo ni mara ya kwanza kwa kiongozi wa kitaifa wa taasisi hiyo kutembelea mkoa huo. Ilikuwa ni furaha kwa wanachama kumpokea kiongozi wao huyo. Kutokana na matatizo ya usafiri ambayo kwa hakika ni matatizo ya kitaifa, kiongozi huyo aliweza kutembelea Katoma, Kilomita chache kutoka Bukoba mjini na Kagenyi iliyoko wilayani Karagwe. Sehemu nyingine hakuweza kuzitembelea kutokana na tatizo hilo la usafiri.

Katika mazungumzo yake na wanachama wa Lajna



*Bi Mwamini Kazema - Sadr Lajna Imaillah Tanzania*

Imaillah, kiongozi huyo aliwaeleza juu ya umuhimu na wajibu wa kutoa michango, kuhifadhi sala na kutimiza ahadi kuhusu jengo la Lajna Imaillah ambalo ujenzi wake unaendelea huko Kitonga.

Wakimueleza matatizo yanayowakabili akina mama hao walimueleza juu ya tatizo sugu linaloambatana na malezi. Jambo hili linakuwa gumu kutokana na ukweli ya kwamba wale wanaoishi nao ni watu ambao desturi zao na utamaduni wao ni kinyume na mafundisho ya dini tukufu ya Islam. Hivyo jitihada zinatakiwa za kupambana na hali hiyo na kuhakikisha ya kwamba Ahmadiyya anaonesha ya kwamba yeye anatekeleza mafundisho ya Kiislam siyo kwa maneno bali kwa vitendo. Tatizo jingine walilomuelezea kiongozi wao huyo linahusu masuala ya ndoa. Lipo tatizo la kuwapata wachumba ambao ni Wanajumuiyya na tatizo hilo linatokana na ukweli ya kwamba wavulana pia ni wachache ambao ni Wanajamaat. Rais wa Lajna alisema ya kwamba hayo si matatizo ya mkoa wa Kagera peke yake, bali ni matatizo ya sehemu nyingi za nchi na hivyo akaahidi ya kwamba kikao cha kamati kuu ya taasisi hiyo kitakaa ili kutafuta suluhisho la tatizo hilo kubwa.

# Hekima ya mavazi mapya katika sherehe ya Idi

*Kutoka uk. 2*

siku sita katika mwezi Shawwal ni sawa na mtu aliefunga mwaka mzima.

Hivyo basi, tunapovaa au kuwavalisha mavazi mapya watoto wetu siku ya sikukuu, huwa tunaashiria katika jambo hili kuwa, kama ambavyo tunavaa mavazi mapya kusitiri miili yetu na pia tunapendeza mbele ya jamii, hivyohivyo tunaashiria kuwa, tunamuomba Allah atuvike khulqa njema, tabia na mwendo wetu uwe ni wenye kumpendeza Yeye na wenye kupendeza katika jamii kwa mwaka mzima. Hiyo itakuwa ndio sababu na maana hasa ya kuvaa mavazi mapya katika siku kuu hiyo. Kwa sababu mwanadamu hata akivaa nguo nzuri namna gani, kama anatabia mbaya na mwenendo mbaya, huyo huwa hampendezi Allah wala hapendezi katika jamii.

Ni juu ya wazazi sasa baada ya kubaini hili kuhakikisha tunawanunulia wanawetu mavazi yanayofaa na kupendeza. Maana mavazi mengine ni vituko, yako yanayobana na kupwaya, na yako ambayo humfanya mtu aonekane kama anapaa n.k. kama mzazi utanunua mavazi ya aina hiyo na kufurahia kuona mwanao ameyavaa, Jamii haitoshangaa kumuona mwanao pindi atakapopevuka amekuwa mwizi, Malaya, mlevi ,muongo, mfitini, fisadi, baradhuli n.k. kwa sababu nguo ulizomnunulia siku ya iddi ilikuwa ni kwa ajili ya kufurahisha macho tu, hukufanya juhudi yoyote ya kumvika mavazi ya Taqwa. Hukumfundisha Qur'an, hakumuhimiza kusali, hakumuhimiza kufunga, kifupi hukumuongoza katika mambo ya dini, mambo ya kumuelewa Mola wake. Kwahiyo juhudi zote unazozifanya za kununua nguo mpya zitakuwa ni bure na hazina maana yoyote iwapo hautamuongoza mtoto kumuelekea Mola wake.Kwani wahenga walisema "Samaki mkunje angali mbichi".

Ni imani yangu sasa kuwa, kama ambavyo tulijazana madukani kujinunulia au kuwanunulia nguo mpya wanawetu, Vivyo hivyo tujazane katika majumba ya ibada na bila kuwasahau watoto. Pia tuwapeleke katika madarasa ya elimu ya dini ili tuwakatie nguo za kiroho zitakazo wasitiri na kuwapendezesha katika siku kuu kabisa kupita zote siku ya hukumu,(**kiyama**).Siku ambayo kila mtu ataulizwa juu ya alichokichunga. Tumuombe Allah atuwezeshe kutekeleza haya. AMIN.

# Kipimo cha kukubaliwa saumu zetu tunacho wenyewe

*Kutoka uk. 12*

kufunga Saumu ya Ramadhani basi inafaa kuangalia kuwa je aliyefunga Saumu amepata makusudio hayo au laa? Mwl. Ramzan alikifahamisha kikao kuwa "Ni kweli Ucha Mungu ni uwanja mpana na hauwezi kupatikana kikamilifu kwa mara moja. Basi ni muhimu kufahamu Ucha Mungu ni kitu gani angalau kwa kusudio la kuelewa maada hii. Ucha Mungu unaweza kusemwa kuwa ni hali ambayo mtu anakuwa nayo katika kujenga uhusiano wake na Mwenyezi Mungu."

Mwalimu aliendelea kufafanua "Ili munielewe nitatoa mfano; Kama mtu atajiunga na dini yeyote ile, siku ya kwanza haiwezikani akalingana kimatendo na waaminio aliowakuta katika dini hiyo. Waaminio hao, kwa siku nyingi inatarajiwa kuwa wawe wamekuwa wakitekeleza ibada mbalimbali ambazo muumini mpya ataanza kwanza kujifunza hatua kidogo kidogo ili aweze kulingana na waaminio wa zamani. Katika hali hii Muuminio Mpya wa Uislamu anaweza kuanza kusali Sala za Faradhi (Sala za lazima) kisha kidogokidogo anaweza kuanza kujua Sala za Suna (Sala zisizo za lazima sana) na Mwisho hujifunza Sala za Nafal (Sala za Hiyari Kabisa)."

Kwa hivyo kila Muuminio inafaa ajikague kila mara baada ya kufunga Saumu ya Ramadhani kuwa "Je hali ambayo amekuwa nayo kabla ya Kufunga Saumu na hali ambayo anakuwa nayo baada ya Saumu inalingana au laa. Kama ndugu ataona kuwa hali yake imekuwa nzuri kiroho yaani kama uwezo wake wa kutekeleza Ibada imekuwa vizuri basi hali hiyo inaonesha kuwa Saumu za huyo ndugu zimekubaliwa. Lakini kama hali yake mara baada ya Ramadhani inakuwa sawasawa au inakuwa mbaya zaidi basi hapo inafaa kuonyesha kuwa Saumu za mtu huyo hazikukubaliwa. Kwani kusudio la kufunga Saumu ni kupata Ucha Mungu yaani kuwa na uwezo wa kutekeleza ibada kwa wepesi zaidi.

Mwl. Ramzan akizidi kufafanua alisema "Hii ndio sababu Wacha Mungu mbalimbali wameeleza kuwa Mwezi wa Ramadhani ni kama Chuo Cha Ucha Mungu ambapo kabla ya Ramadhani Mtu anatakiwa ajikague na kuona udhaifu wake upo wapi? Kisha katika mwezi huo basi ajitahidi kuuondoa udhaifu huo. Mfano Mzuri ni kama Mtu ataona kuwa anaudhaifu wa kusema uongo basi Katika mwezi huo ajitahidi kujiepusha kusema uongo. Hivyo kama mtu ataachana kabisa na khulka ya kusema uongo basi mtu huyo afahamu kuwa Saumu yake imekubaliwa. Na hali hii ya kutosema uongo ikiendelea maisha mazima ya ndugu huyo basi mtu huyo atakuwa kweli kabisa amefaulu katika Saumu yake na kwa hiyo mwaka unaofuata atachagua kupunguza udhaifu mwingine na hivyo kila mwaka hali yake ya Ucha Mungu itazidi.

KULINGANA NA WACHAMUNGU WA KABLA YETU:

Kigezo cha pili ambacho kinaweza kutusaidia kutambua kuwa Saumu zetu zimekubaliwa ni kuwa "Inafaa kuangalia kuwa je hali tunazokuwa nazo baada ya Saumu zetu ndizo hali walizokuwa nazo Wacha Mungu wa zamani waliokubaliwa ibada zao au laa?" Kimsingi kama Lengo la Saumu ni kutufanya tuwe Wacha Mungu basi inafaa tuwe na hali na sifa ambazo Wacha Mungu wa huko nyuma Wamekuwa nazo.

Akifafanua kigezo hiki Mwl. Ramzan alisema "Mwanzoni mwa hutuba yangu nimesoma Sura ya 5 aya ya 28 ambapo Mwenyezi Mungu ameelezea tukio moja la kale ambapo Watoto wawili wa Adamu walitoa Sadaka (yaani walitekeleza ibada Fulani) kisha ya mmoja ikakubaliwa na ya mwingine haikukubaliwa. Basi yule ambaye Sadaka yake haikukubaliwa alimwambia mwenziwe kuwa nitakuuwa na yule ambae sadaka yake ilikubaliwa alisema kuwa 'Mwenyezi Mungu huwakubalia Wamchaoo tu na kama utanyanyua mkono wako kuniua mimi sitanyanyua mkono wangu na kukuua bali nitakuacha ujichukulie dhambi zangu na zako'. Na kwa hiyo yule Mcha Mungu hakuwa tayari kuvunja Amani na akaonyesha uvumilivu wa hali ya juu."

"Katika habari hii mmeelezwa hali ya pekee ya Wacha Mungu ambapo wao wamekuwa wavumilivu sana na wamekuwa hawakubali kuvunja Amani wakati wowote ule. Na hivi ndivyo Historia ya Wacha Mungu mbalimbali imekuwa. Kwa hivyo kama kila kundi la Waislamu au wanadini wataonyesha hali hii basi Amani (Mungu Akipenda) itaenea na Serikali zetu zitaweza kuwatambua wahalifu kwa urahisi kuliko kama kila mmoja atachukuwa Sheria mkononi na kuanza kufanya vurugu na kusababisha vifo vya watu chungumzima."

"Hali kama hii imepatikana huko Pakistani ambapo watu wa dini moja kila mara wamekuwa wakitekeleza ibada lakini kila Watu wamekuwa wakijichukulia Sheria Mkononi zidi ya kundi lingine kiasi ambacho imekuwa ni vigumu kutambua Wacha Mungu na Wasio. Lakini kama vile Jumuiyya ya Waislamu Waahmadiyya wamekuwa wakionyesha Subira na Staamili ya hali ya juu imekuwa kila walipo fanyiwa ubaya wao wameshika Subira kama Mtoto yule wa Adamu alivyoonesha Subira. Na kwa hivyo tunaweza kusema kuwa wao ndio wanaopokelewa Ibada zao."

HEKIMA YA NENO IDD

Neno IDD linatafsiri kuwa 'Ni Siku ya furaha na ni yenye kujirejea rejea'. Hekima ya neno hili linaonyesha kuwa ni juu ya Waaminio kuona kuwa hali za kupokelewa kwa Ibada zao linatakiwa lisiwe la mara moja tu. Mwl. Ramzan alisema "Waaminio wanapaswa kuona kuwa Faidi za Ibada zao au kama zao, zimeendelea kuzalisha Wacha Mungu katika kila zama. Ni hapo tu ndio juhudi za Binadamu zinapoweza kuongezeka ama sivyo kama ilivyotokea katika Nyimati zilizopita Binadamu hukata tamaa na kutekeleza Ibada na mwisho wanafika mahali pa kuamini kuwa hakuna faida yeyote katika kutekeleza Ibada zilizofundishwa na Manabii wao. Katika hali kama hii, Wafuasi wa dini hizo huanza kuamini kuwa Neema zozote za kiroho hazipo na kwa hivyo huamini hakuna Nabii au aina yeyote ya wateule wa Mungu watawafikia kutoka kwa Mungu katika zama zao."

"Hivi ndivyo ilivyo tokea leo, waaminio wa dini mbalimbali wamefika mahali paa kuamini kuwa hakuna Mteule yeyote kutoka kwa Mwenyezi Mungu anaweza kutufikia. Na kwa tathmini hii hawawezi kupata Furaha ya Kweli. Tunaona jinsi ilivyotokea mara baada ya kifo cha Mtume Muhammad (s.a.w), Abubakar (r.a) Akateuliwa kuwa Khalifa na tunaona jinsi Waaminio walivyopata Faraja ya Kweli".

"Leo ni katika Jumuiyya ya Waislam Waahmadiyya pekee, hali kama hii inapatikana. Nasi tunatakiwa kudumisha hali hii na kila mara mmoja wetu anapoteuliwa kushika nyadhifa Fulani ni juu yetu kuungana nae. Kama mmoja wetu atateuliwa kuwa Raisi wa tawi basi tushirikiane nae na tusiseme kuwa huyu mbona halingani na Fulani. Ni kwa namna hii tu Ndio tutanufaika na Ukhalifa. Ikumbukwe kuwa Ukhalifa umeahidiwa kudumu lakini asiyeshikamana nao yeye ndio atatupwa nje ya Ukhalifa."

UMUHIMU WA SIKU YA IDD:

Naye Mwl. Abdallah Mbanga katika hutuba yake akifafanua maada aliyopangiwa iliyokuwa inahusu 'Umuhimu wa siku ya Idd' alisema "Umuhimu mkubwa wa siku ya Idd ni kutukumbusha Waaminio kuwa tunatakiwa kuhakikisha kuwa yale yote tuliyoweza kutekeleza katika Mwezi wa Ramadhani tunaendelea kutekeleza baada ya Ramadhani. Na juhudi yetu kubwa iwe katika kutafuta Ucha Mungu zaidi na zaidi nasi tuweze kupata mafanikio ya kiroho ili tuweze kuona jinsi hadithi ile ya Mtume (s.a.w) inavyo timia. Wakati aliposema kuwa 'Mtu anayefunga Saumu hupata faraja mbili ya kwanza ni wakati ule anapokuwa anafungua saumu yake na ya pili ni wakati atakapo kutana na Mola wake Mtukufu."

Mwisho hafla hii ilimalizika kwa Mwalimu mpya wa tawi la Kitunda, Mwl. Mussa Said Siamini, kwa kutoa hotuba ya shukrani na kuongoza maombi ya kimya kufunga hafla yenyewe.

# TAARIFA YA IJTIMAA YA ANSWARULLAH 2013

*Na Ustadh Khamis Wamwera,*
*Katibu wa Habari Ansarullah*

Inshallah Ijtimaa yetu itafanyika kama kalenda yetu inavyoonyesha. Hapana shaka itakuwa mnamo tarehe 14 hadi 15 ya mwezi wa Disemba 2013. Kama kawaida itafanyika kwenye eneo letu kule Kitonga mjini Dar es salaam. Sadr Sahib, Muadham Inayatullah S. Nakuchima, anawataka Answarullah wa nchi nzima wahudhurie bila kukosa hata mmoja. Udhuru wa kutengenezwa usiwepo. Anasema kwamba kufika kwa kila mmoja wetu ndiyo mafanikio ya Ijitimaa.

Ukweli ni kwamba hadi sasa, tuna matawi mengi tu nchini hapa. Kufuatana na Tajnid ya mwaka juzi tuna matawi takribani zaidi ya 240. Kwa hesabu hii tu inatutia moyo hasa kama kila tawi kwa akali lilete Answar wawili tu, Ijtimaa yetu itatia shani, kwa mahudhurio. Tunaomba iwe hivyo na zaidi.

Muda umepita sana na siku zinakaribia mno. Na Aswarullah kuanzia sasa wajipange vizuri na waandae vyema safari yao ya kuja kwenye Ijtimaa. Watayarishe nauli zao za kwenda na kurejea nyumbani huko kama kawaida. Mazaim wa matawi, Manazim wa mikoa na Kanda wahakikishe kwamba kila tawi linaleta Anwarullah wawili au kama watakakosa, hata huyo mmoja atatosheleza. Pasibaki tawi lolote nyuma. Kutomleta mjumbe, ni kusinzia katika safari yetu ndefu ya kuelekea kwenye ufaulu na ushindi.

Fanyeni mpango hata wa kumchangia mmoja wenu hapo tawini ili ahudhurie kwenye Ijtimaa ya Tanzimu yetu kwa niaba yenu. Kwa hakika anayemuogopa Mwenyezi Mungu kwa dhati hataona hasara wala ubaya kujitolea katika njia yake. Mwishoni mwa mwezi Septemba mwaka huu, tulifanya Jalsa yetu ya mwaka. Tunaweza kusema mahudhurio hayakuwa mazuri sana. Wanajumuiyya hawakuitikia vilivyo wito kutoka kwenye matawi yao. Ni Wanajumuiyya walewale wa kila mwaka ndizo sura zilizoonekana. Kwa nini sura mpya matawi hazikuleta?

Naam, tunawakumbusha Answar wa Dar es salaam, uzoefu wetu umebaini kwamba wanachama wetu wa Mkoa huu wamekuwa wazito sana, hivi kwamba mahudhurio yao kwenye Ijtimaa kila mwaka yanakuwa si ya kuridhisha. Wanaojitokeza huwa wachache mno, kitu ambacho hakileti taswira nzuri. Mkoa wa Dar es salaam una Aswarullah zaidi ya 150, lakini wanaohudhuria kwenye Ijtimaa yetu huwa nusu ya hao. Kwa nini hasa?

Tunamhimiza Nazim wa mkoa wa Dar es salaam na Mazaim wake wathibitishe kila Answarullah anahudhuria kwenye Ijtimaa ya mwaka huu bila kukosa. Tuone haya jamani, maana haya ni sehemu ya imani. Ikiwa Answarullah kutoka Bukoba, Kigoma, Ruvuma, Sumbawanga, Mbeya, Pemba na Unguja ambao wana msafara mrefu, bali pia wanatumia fedha nyingi za nauli na masurufu wanafika kwenye Ijtimaa kila, kwa bashasha na furaha ya ajabu, je wewe wa papa hapa Dar es salaam unatatizwa na kitu gani mpaka unashindwa kuhudhuria kwenye Ijtimaa? Ni swali ambalo kila asiyehudhuria katika Ijtimaa ajiulize binafsi na kulipatia jibu sahihi.

Hatukatai, udhuru unaweza kupatikana pengine kwa ghafla, kama hali hiyo itapatikana, Ofisi ya Sadr wakati wote ipo wazi. Tafadhali mweleze Sadr Sahib tatizo lako hadi ukashindwa katika Ijtimaa. Ndiyo Nizamu ambayo Answarullah wakati wote wanatakiwa kuitolea mfano kwa makundi mengine. Lakini kunyamaa tu kimya bila maelezo yoyote haipendezi. Mtindo huo uko mbali sana na Nizamu ya Tanzimu yetu.

Answarullah wa mkoa wa Dar es salaam wanatakiwa kuelewa vizuri sana kwamba wao ndio wenyeji halisi wa Ijtimaa. Wao wana haki na wajibu mkubwa wa kuwapokea wageni wa Seyidna Ahmad (as) wanaotoka m ikoa mbalimbali na kuhudhuria katika Ijtimaa. Haipendezi wala hainogi wenyeji kuwa goi goi kiasi hiki hata sisi kuthubutu kukumbusha.

Jitokezeni kwa wingi na muwakaribishe wageni wanaotoka nje ya Dar es salaam. Tunajua na ni kweli kwmaba baadhi ya Answarullah ni waajiriwa mahala fulani, kama hivyo ndivyo, ni wakati muafaka kwa hivi sasa kila mtu afanye mipango kazini kwake kupata ruhusa kwa hizo siku tatu, Ijumaa, Jumamosi na Jumapili.

Pia kila Answarullah ahakikishe michango yake ya lazima anatoa bila kukosa, Chanda Aam, Chanda Jalsa, Chanda Tahrik-e-Jadid, Chanda Waqf-e-Jadid, Chnda Answarullah na Chanda Ijtimaa. Ni michango iliyo wajibu kwetu. Kila mmoja aithibitishie nafsi yake mwenyewe kwamba anashiriki bila kukosa michango hii na mingine ya Jumuiyya na Tanzimu.

# Kila Ahmadiyya atekeleze wajibu wake

*Kutoka uk. 10*

kwamba wao pia wanapaswa kutimiza majukumu yao na mojawapo ya majukumu hayo ni kwamba wanapaswa kufanya mipango ya ufundishaji wa Quran katika matawi yote. Wanapokuwa wanazitembelea jamaat matawini wajaribu kuwafundisha waalimu ambao wataweza kuwafundisha wanajumuiya Kurani Tukufu. Madrasa hizi ziwe za kudumu, mara moja au mbili tu kwa wiki haitoshi. Wakati wa Magharibi au Isha madrasa hizi zaweza kufanyika. Kama mbashiri hayuko safarini, na mwenyewe yupo, anapaswa kuendesha darsa yeye mwenyewe.

Malalamiko mengi yananijia kwamba hatuna mtu yeyote anayeweza kuwafundisha watoto wetu Kurani Tukufu na tunalazimika kuwapeleka watoto wetu kwa wasio Waahmadiyya. Hivyo kuna haja kwa watoto kufundishwa Qaida Yassarnal Quran. Kwa kufanya hivyo watapata faida ya ziada ya kuwazoeza msikitini na hii itakuwa na matokeo yenye manufa sana kwani kufundisha Quran kumejaa baraka ambazo ziko wazi kwa kila namna.

Wabashiri wanatakiwa pia kukumbuka kwamba kwa kawaida huwa wanahama kituo cha kazi kila baada ya miaka mitatu au minne hivi na ikilazimika katika muda mfupi chini ya huo. Nimesikia kutoka baadhi ya nchi kwamba kuna ukaidi unaoonyeshwa wakati mwingine. Wanapaswa kulipokea hili kwa furaha, kwa fadhili za Allah angalau jambo hili mimi sijalishuhudia hapa Uingereza.

Ni muhimu vile vile kukumbuka kwamba kama ni lazima kumtanabahisha Amir juu ya jambo fulani la muhimu ambalo lahusikana na itikadi takatifu za Jamaat au linalohusikana na maamrisho ya sharia, unapaswa kufanya hivyo kwa taadhima na kwa heshima. Lakini kama ushauri haukupokelewa na uharibifu ukawa unafanyika kwa Jamaat au kanuni za sheria zikiwa zinavujwa hapo kwa namna yoyote nipewe taarifa. Hakutakiwi kuwepo haja ya aina yoyote ya mabishano au kugombana kwa namna yoyote – kwa kuwa mambo kama hayo huwa chanzo cha kuleta utengano ndani ya Jumuia. Ni kweli kwamba nimeshawahi kusema kuwa Wabashiri (walimu) wanaweza kuwakumbusha Maamiri/Viongozi juu ya matakwa ya sharia na kadhalika, lakini hili halina budi lifanyike kwa kuzingatia agizo hili.

Mwenyezi Mungu na Atuwezeshe sote kuwa Waahmadiyya wa kweli na Atuwezeshe kutimiza majukumu yetu yote kikamilifu. Amin.

Baada ya sala ya ijumaa nitaongoza pia sala ya jeneza ya ghaibu ya marehemu bibi Tania Khan, mke wa Bwana Asif Khan aliye katibu wa mambo ya nje ya jamati ya Kanada. Mnamo tarehe 6 Augusti 2013 alifariki akiwa na umri wa miaka 38. *Inna lillahe wa innaa ilaehe rajeuuna.* Alikuwa mwenye asili ya Lebanon. Mnamo mwaka 1998 alijiunga na Jumuiyya ya waislamu waahmadiyya na alikuwa mhubiri mkubwa wa jumuiyya mwenye shauku kubwa ya kufanya mahubiri. Pamoja na kuwa katibu wa tabligh wa kitaifa wa kinamama, Alipata kuitumikia Jumuiyya katika nyadhifa mbali mbali. Alikuwa mwanachama wa kudumu wa MTA Kanada, na siku zote alikuwa tayari kufikisha ujumbe wa Ahmadiyya na wa kiislamu katika vyombo vya habari. Kwa shabaha hiyo, alisafiri sana mashariki na magharibi ya Kanada na hata aliwahi kwenda marekani. Alikuwa mwenye kueleza mtazamo wake kwa uzuri na namna yenye kuvutia katika kila ngazi. Alikuwa ni mwalimu wa shule na hivi karibuni alichaguliwa kuwa naibu wa mwalimu mkuu wa shule. Alijitahidi sana kuwafundisha wanafunzi wake maadili mema na akapata tuzo kadhaa kama mwalimu. Alikuwa na uhusiano imara sana na Ukhalifa na alikuwa akijitahidi kufuata kila mpango uliotangazwa. Alikuwa mwenye kuvaa hijabu na kujawa na jadhba za kuwahudumia wanadamu wenzake.

Alikuwa ameto a wasia wa kujitolea baadhi ya sehemu za (viungo vya) mwili wake na alikuwa anawahurumia sana mafukara. Alikuwa mke na mama asiye na kifani na alijitahidi kutimiza haki ya kila kitu. Ingawaje aliolewa na mpakistani, lakini alijibadilisha na kuishi na mumewe kwa furaha. Alikuwa ni mwanamke mwaminifu mwenye kulinda desturi za kiislamu. Alikuwa amejiunga na nidhamu ya wasia na kwa fahili za Mwenyezi Mungu mabinti zake watatu ni waaqifaate nau (watoto waliotolewa waqfu kabla ya kuzaliwa kwao). Alikuwa anajulikana sana, ndio sababu waziri mkuu wa jimbo aliye mwanamke, wabunge, madiwani, wanafunzi, waalimu na wasiokuwa waahmadiyya walikuja, kwa wingi sana, kushiriki katika mazishi yake. Alipendwa na kila mmoja na alikuwa na umaarufu mkubwa sana. Nimesikia sifa zake kutoka kwa watoto na wakubwa. Mwenyezi Mungu Amghofirie na kumnyanyua madaraja na kuwajaalia mabinti zake na mume wake subira na nguvu. Amin.

**Mwisho**

# Ansarullah waambiwa wafanye kazi za Jumuiya kama nyuki

*Kutoka uk. 12*

hao waliofika, aliweza kushiriki kila kipindi hadi kikao cha mwisho wa Semina.

Semina ilifanyika chini ya uwenyekiti wa Naib Sadr Bw. Abdullah bin Nassoro. Baada ya kusomwa Qur'an Tukufu na Bw. Sudi Shabani Jaka, kisha kiapo kilichoongozwa na Bw. Kasimu M. Maftah na kufuatwa na shairi lililoghaniwa na Bw. M. A. Likoko; Muavian Sadr I Bw. Salum Dadi Mtamila alisoma Khutuba ya ufunguzi wa Semina iliyotayarishwa na Sadr Sahib mwenyewe Muadham Inayatullah S. Nakuchima.

Katika Khutuba hiyo Sadr sahib, aliwashukuru Answarullah wote waliohudhuria kwenye Semina kwa kuacha shughuli zao za kujipatia riziki na kuweza kushiriki kwa pamoja katika Semina hiyo. Alisema kwamba huo ndiyo moyo wa kujitolea na kutanguliza dini mbele ya dunia, moyo ambao kila mmoja wetu anatakiwa awe nao. Pia Sadr Sahib katika Khutuba yake hiyo aliwataka wanasemina kuzingatia kwa makini yale yote watakayofundishwa na waalimu ili wakitoka hapo wawe wameiva barabara na ili nao wakawe waalimu kwa wengine, Sadr aliwaambia wanasemina kwa kuelewa mambo mbalimbali, Answarullah wanaweza kuitumikia vyema Tanzim na Jumuiyya kwa jumla.

Baada ya khutuba hiyo ya ufunguzi, panziya ya Semina ilifunguliwa. Kwa muda wa siku hizo mbili zote masomo muhimu zaidi ya kumi yalifundishwa. Mkufunzi Mkuu Bw. Ramzan Fazal kama kawaida alianza shughuli kwa kuwakilisha kwa wanasemina somo la mfumo wa uongozi katika Tanzim yetu. Kadhalika alifundisha somo la majukumu yanayojuzu, uendeshaji wa vikao vya Tanzim na namna ya kuchukuwa Bajeti. Somo la Tajnid (Sensa) na somo la ufuatiliaji michango, yalifundishwa na Bw. Abedi Idi ambaye ni Nazim wa Mkoa wa Dar es salaam na Qaid Tabligh wa Taifa katika Tanzim. Somo la Taarifa ya Zaim liliendeshwa na Muavian Sadr - II Bw. Salum Dadi Mtamila.

Kikao cha mwisho cha Semina kilikuwa siku ya Jumapili ya tarehe 25/08/2013. Kikao hiki kilianza mnamo saa 8:30 kwa usomaji wa Qur'an Tukufu iliyosomwa na Bw. Sudi S. Jaka na kufuatiwa na shairi lililoimbwa na Bw. N. Bagula. Kisha ilifuata khutuba fupi ya kumkaribisha mgeni rasmi. Khutuba hii aliitoa Naib Sadr - I Bw. Abdullah Nasoro ambaye alimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kufanikisha Semina kwa salama na amani, bila kutokea tukio lolote baya. Pia aliwashukuru wenyeji kwa kuchukua uzito wa kuwapokea wanasemina na kuwa nao kwa muda wote wa siku zote mbili hizo. Hayo, alisema, yanatokea kwa sababu wanajumuiyya wanaipenda dini.

Mgeni rasmi ambaye ndiye alifunga semina hii alikuwa Mbashiri na Mwalimu wetu wa Ifakara. Ni Mwl. Mahmood Chilembwe. Yeye katika khutuba yake kwanza aliishukuru Tanzim ya Answarullah kwa kumfanya yeye awe mgeni rasmi katika kufunga semina yao, ijapokuwa hajafikia uanswar. Alisema amepokea heshima hiyo kwa sababu Tanzim iliona anafaa. Ndipo Mwalimu Mahmood Chilembwe akawaambia wanasemina; wote tumo kwenye chombo kimoja. Tukiangalie na tukitunze vilivyo. Ni Jumuiyya ya Ahmadiyya. "Answarullah muwe mfano mwema katika Tanzim zetu tulizo nazo, bali fanyeni kazi kama nyuki". Nyuki, alisema Mwalimu; "Wanatoa mafunzo mazito kwa watu wenye akili. Nyuki ni viumbe wadogo sana, lakini ni jeshi lenye nidhamu ya hali ya juu sana. Wanafanyazi kwa pamoja na wanaongozwa na Malkia wao nao wanafuata amri".

Mwalimu Chilembwe kwa mara nyingine aliwashukuru viongozi wakuu wa Tanzim ya Answarullah kufanyia Semina kule Ifakara. Ni changa moto tosha. Kwa siku mbili hizi tu, Ifakara imepata khabari njema.

Alihitimisha

Maoni ya waliohudhuria Semina;

Naib Sadr Saf Dom, Bw. Mwinyimvua Usi alisema kwamba kwa kweli masomo hayo ni changamoto kubwa sana katika Tanzim yetu. Kama kila Answarullah atatekeleza wajibu wake, shughuli na mambo yetu mengi kama si yote yataenda vizuri. Alipendezwa kuona Answarullah wawili ambao walikuwa na umri mkubwa kabisa, lakini walishiriki kwenye semina hiyo kwa muda wote wa hizo siku mbili.

Mwinyimvua Sahib aliwaomba wanaanswarullah wote kupitia kwenye Semina hii kuwa ni lazima na inatupasa kujipatia elimu ya Tanzim yetu na kuifanyia kazi barabara. Iwapo kila mmoja wetu atakuwa tayari kwa hilo, basi shughuli za Tanzim zitakwenda motomoto. Wanasemina wenyewe kwa ujumla wao walifurahi sana kupokea masomo mbalimbali yaliyosomeshwa. Waliona siku mbili hizo za Semina zilikuwa chache mno. Lakini hata hivyo walikiri kwamba walichokipata hapo ni muhimu sana ambacho kabla hawakuwa wanakijuwa. Kwa hicho walichokipata kitaongeza uwezo na nguvu ya kufanya kazi za Tanzim vizuri zaidi.

# ADABU ZA MSIKITINI

*Kutoka Idara ya Malezi*

1. Msikiti ni sehemu ambayo ibada ya Kiislamu inafanyika, inatumika kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Pia inatumika kama sehemu ya mikutano ya masuala ya kidini. Hakuna kinachotakiwa kwa kuivuruga hiyo.
2. Mtu anatakiwa aidha afanye ibada au ajiweke katika hali ya kumkumbuka Mwenyezi Mungu au watu wazungumzie masuala ya dini pekee. Lakini maongezi yao yasiwasumbue waliokuwa kwenye ibada.
3. Wakati mtu anapoingia Msikitini anatakiwa aombe dua ifuatayo;
*"Bismillahis Salaatu Wassalaam al'aa rasuulillah, Allahummagh Fir-lii zunubii waftah-lii abwaba rahmatika".*
4. Pia usali rakaa mbili za nafal unapoingia Msikitini, itakuwa kama shuQur'an mbele ya Mwenyezi Mungu Ambaye Atakuwezesha uufikie Msikiti kwa khulka njema. Hiyo ni tunu kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.
5. Kama mtu anasali, hautakiwi kupita mbele yake. Ila unaweza kupita mbali kidogo kutoka sehemu anayosujudu.
6. Ni kitu kisichofaa mtu kuongea kwa sauti Msikitini au kufanya kitu kisichopendeza ambacho kinawasumbua waliopo kwenye sala kwa muda huo.
7. Msikiti unatakiwa wakati wote kuwa safi, kama inawezekana manukato yatumike ili kuifanya sehemu inayokubalika. Hakuna uchafu unaotakiwa kuachwa Msikitini, unatakiwa uondolewe haraka iwezekanavyo.
8. Hautakiwi kula chochote ambacho kinatoa harufu mbaya kabla ya kuingia Msikitini, harufu ya mdomo wako itawasumbua wengine.
9. Usiteme mate ndani ya Msikiti au sehemu zake zinazotumika kwa kazi maalumu.
10. Usijiingize kwenye uuzaji au ununuaji wa biashara Msikitini, pia usizungumzie masuala ya biashara Msikitini.
11. Jambo lisilopendeza ni kutoa tangazo la kitu kupotea ndani ya Msikiti. Ikitokea kitu kimeachwa na kupotea Msikitini tangazo lina ruhusiwa kutolewa ndani ya Msikiti.
12. Wale waliochelewa hawatakiwi kuwaruka watu wengine kwa ajili ya kwenda safu za mbele.
13. Watoto wadogo kabisa wanaoweza kupiga kelele na kukojoa ndani ya Msikiti wasiletwe ndani ya Msikiti.
14. Imamu atoapo hotuba ya Ijumaa, wasikilizaji wanatakiwa wawe watulivu na yasiwepo mazungumzo yanayoendelea. Ikitokea kumtuliza mtu anayezungumza, asiambiwe kwa maneno, bali kwa kumgusa na kumuonyesha aache mazungumzo.
15. Wakati unapotoka Msikitini unatakiwa kuomba dua ifuatayo;
*"Bismillahis Salaatu Wassalaam al'aa rasuulillah, Allahummagh Fir-lii zunubii waftah-lii abwaba rahmatika".*

# Kila Ahmadiyya atekeleze wajibu wake

*Kutoka uk. 11*

kwa hivyo ikalazimika hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi yao na wakalizimika kufanya shughuli zao chini ya uangalizi fulani. Wakati uchunguzi zaidi ulipofanyika ikabainika kwamba wengi wao ni watu ambao hawasikilizi khutba na wengi wao hawashiriki kikamilifu katika kujiweka karibu na Jamaat, siku hata siku na wala hawashiriki katika hafla mbali mbali za Jumuiya.

Lakini kwa kuwa walikuwa nao uhusiano wa kina na Jamaat ndani ya damu zao, ambao ulikuwa ni sehemu ya utu wao, basi pale walipotakiwa kutii mipaka fulani fulani waliyowekewa, na wakapewa adhabu kidogo, walipata woga na hofu na wakaanza kuandika barua za kuomba radhi na kuomba msamaha wakionyesha hofu kubwa na woga. Wengine walikuja pia kuonana nami. Na katika nyakati kama hizo walifikia hadi kulia. Kama wangalikuwa na mawazo ya kidunia tu, hii isingeliweza kuwa hali yao.

Kwa hiyo wapo watu kama hawa, ambao kwa sababu ya mambo ya kidunia na pirika zake wanakuwa sio waangalifu kwenye wajibu wao wa kidini, lakini wanapoelekezwa kwenye mambo haya huonyesha kupatwa na haya na wanaanza kuomba masamaha wa Mungu na huanza kutubu na kuonyesha mahusiano na kujishughulisha na Jamaat. Kwa hiyo kazi hii ya kukumbusha na kuelekeza fikra za watu kwenye mambo haya ni sehemu ya kazi ya mfumo wa nidhamu ya Jamaat – Nidhamu ambayo imeundwa na makatibu na wabashiri na waalimu na watumishi wengine – hii ndio kazi ya hao wote.

Jaribuni kuzidisha mahusiano binafsi baina ya kila Mwanajumuiya na Ukhalifa. Jaribuni kuamsha katika moyo wa kila mwanajumuiya mapenzi na uaminifu na utii kwa Ukhalifa. Hali hii ipo katika nyoyo zao lakini pale wanajumuiya wanapokumbushwa na kutiwa moyo hali hii hung'aa vizuri zaidi na kama uchafu fulani umedondoka kwenye mapenzi haya na maungano na Ukhalifa, kwa kukumbushwa uchafu huo hutoweka. Ikiwa idara ya tarbiyyta (malezi) itaendelea kuwatia shime wanajumuiya ili waonyeshe uhusiano wao na Ukhalifa na kuendelea kuwahamasisha kushiriki katika mipango na matukio mbalimbali ya Jamaat, hapo tutaona kwamba kadri mahusiano yao na ukhalifa yanavyoimarika matatizo mengi ya kimalezi yatakuwa yanatatuka.

**Suala linalofuata ambalo nataka kuzielekeza fikra za kila mmoja wetu ni haja ya kuweka wazi kwa kila Muahmadiyya wajibu wake kuhusu kujitolea kifedha – chanda/michango**.

Kumbukeni kwamba kujitolea michango sio kodi. Kwa hakika kujitolea kifedha ni moja ya majukumu ambayo yametajwa tena na tena katika Kurani Tukufu. Kwa mfano Allah Mtukuka anasema mahali fulani:

[64:17] *Kwa hiyo Mcheni Mwenyezi Mungu mwezavyo, na sikilizeni na tiini na toeni, itakuwa heri kwa nafsi zenu; na aepushwaye na ubahili wa nafsi yake, basi hao ndio wenye kufaulu*.

[64:18] *Mkimkatia Mwenyezi Mungu sehemu nzuri, Atawazidishieni na Atawaghofirieni, na Mwenyezi Mungu ndiye Atoaye thawabu nyingi, Mpole,*

Kwa hiyo ni dhahiri kutoka katika aya hizi kutoa katika njia ya Allah ni jambo muhimu kabisa kwa mwaminio. Ni wale tu wanaotoa katika njia ya Mwenyezi Mungu ndio watakaopta ufaulu. Na inasemwa kwamba kutoa katika njia ya Allah ni kama vile umemkopesha Allah. Na Allah ni yule ambaye hurejesha kile alichokopeshwa kikiwa kimeongezeka kwa mara nyingi. Na watu wananiandikia matukio mengi kama hayo kwamba tulitoa chanda kiasi hiki katika njia ya Allah na Allah aliturudishia kiasi kile kikiwa kimeongezeka mara nyingi na mara kwa mara nimetaja matukio kama hayo.

Allah ni Ghani – Anayejitosheleza, na hana haja ya fedha zetu. Kwa hakika hii ni kwa ajili ya kututakasa na kuangalia kiwango chetu cha utii, na kutuona tunapiga hatua katika njia za utawa, na kuona ni kwa kiasi gani tunatekeleza ahadi zetu za kuwa tayari kujitolea katika njia yake.

Mwenyezi Mungu Anatuita kutoa matumizi katika njia yake ili kuifanya dini Yake isambae kila mahala. Kila Ahmadiyya inambidi aelewe kiini hiki cha kutumia katika njia ya Mwenyezi Mungu ambayo ndio sababu ya kutoa michango yetu.

Ikiwa tunatoa chanda kumfurahisha katibu fulani wa fedha au rais wa jamaat fulani au kumuondoa mgongoni mwetu (yaani asitufate fate) hapo hakuna thamani yoyote ya utoaji kama huo wa chanda. Inakuwa bora kwa mtu kama huyo asitoe kabisa chanda.

Kama unatoa chanda kwa kushindana na mtu fulani ili tu kumuonyesha kwamba wewe unatoa zaidi kuliko yeye, hii pia haina faida yoyote. Kwa kifupi sababu yoyote tofauti na ile ya kutaka radhi ya Allah ni batili na yeyote anayetoa chanda ni lazima wakati wote afikirie kwamba kwa hakika hii ni rehema na hisani ya Allah juu yake kwamba amempatia uwezo wa kutoa katika njia Yake, badala ya kufikiria kwamba kwa kutoa chanda mtu anamsaidia Mungu au Jamaat.

Kwa hiyo kila mmoja anayetoa chanda ni lazima aweke akilini kwamba kwa kufanya hivyo anajaribu kupata kukubaliwa na Allah na kupata radhi yake. Kujitolea kifedha ni jambo la muhimu sana kwa Jamaat zilizoanzishwa na Mungu, Hii ndio sababu nimeeleza kwa jamaat zote kwamba ni lazima wajitahidi ukomo wa jitihada zao kuona wanajumuiya wapya wote na watoto wanashiriki katika kujitolea kifedha kwenye Waqfe jaded na Tahrik jaded hata kama wafanye hivyo kwa kutoa pesa moja, ili kwamba wajenge tabia ya kutoa na wawe wenye kuweza kupokea rehema na hisani ya Allah.

Akizungumzia umuhimu wa michango mahali fulani Masihi Aliyeahidiwa (a.s) anasema:

Katika dunia tunaona kwamba mtu anapenda sana mali. Ndio maana imeandikwa katika vitabu vya taawili za ndoto kwamba ikiwa mtu anaona katika ndoto ametoa ini lake kumpa mtu fulani basi hii inamaanisha mali. Ndio maana inasemwa kwa ajili ya kupata uchamungu wa kweli na utawa:

*[3:93] Hamtaweza kuufikia wema hasa mpaka mtoe katika vile mnavyovipenda;*

Ukweli ni kwamba huruma kwa binadamu inahusisha kutumia kwa ajili yao mali zetu, na mpaka pale mtu anapotumia mali yake kusaidia binadamu na anajitolea muhanga kwa ajili ya hili, imani ya mtu bado haijatimia. Mtu atawezaje kuwa wa manufaa kwa mwingine bila kujitolea. Ili kuwa wa manufaa kwa wengine kujitolea ni lazima. Na katika aya hii kujitolea huku huku kumetajwa. Kwa hiyo kutoa kwa ajili ya huduma kwa wanadamu ni kipimo cha kiwango cha ucha Mungu wa mtu na utawa. Kiwango hicho kilionekana wakati wa maisha ya Abu Bakar r.a. pale Mtume Mtukufu s.a.w. alipoeleza haja ya kujitola yeye akaleta kila kitu kilichokuwemo kwenye nyumba yake na kumpatia (Mtume s.a.w.).

Kwa hiyo ni muhimu kwamba makatibu wa fedha wa Jamaat wawafunze wanajumuiya kwa namna hii na kuwaambia kwamba ucha Mungu wao na imani yao inaimarika kupitia kujitolea kifedha. Hali kadhalika Wabashiri vile vile wanapaswa kuwaasa Wanajumuiya juu ya hili kila wanapopata nafasi ya kufanya hivyo. Hili linahitaji kuzingatiwa kwa kudumu.

Makatibu wa fedha kwenye kila ngazi wanahitaji kuchangamka. Wajibu wao ni kutimiza majukumu yao na wanatakiwa kuwa na njia maalum kwa ajili ya kumfikia kila mmoja. Haitakiwi kwamba kazi hii iachwe kwa viongozi wa tanzeem tu kwamba wao ndio waitekeleze. Watumishi wa tanzeem wanaweza kusaidia tu kwa namna ya kuwahimiza wanatanzeem wao, zaidi ya hapo si kazi ya Tanzeem. Tanzeem zinaweza kuzielekeza fikra za wanachama wao na kuwaomba watoe ushirikiano kwa makatibu wa fedha na kuwaelekeza juu ya dhana ya kutoa chanda. Ni kazi ya makatibu wa fedha kwamba wajaribu kuifikia kila nyumba na kila makazi.

Siku hizi kuna urahisi mwingi (wa mawasiliano) na hasa hapa Ulaya. Huko Pakistan walikuwepo makatibu wa fedha ambao walifanya kazi kutwa nzima kisha wakatumia wakati wao wa jioni kuwatembelea watu katika nyumba zao … katika miji mikubwa kama Lahore na Karachi kwa kutumia baiskeli walikuwa wakionekana kupita nyumba hadi nyumba, wakiwaasa watu na kuwaelekeza kwenye mambo haya.

Hapa (Uingereza) kuna urahisi mwingi lakini bado (makatibu wa fedha) hawatimizi kazi zao kama inavyopaswa kufanyika na ninapokea baadhi ya ripoti kwamba baadhi ya hawa makatibu wa fedha wao wenyewe sio watoaji wa michango kwa kiwango kinachohitajika. Iwapo michango yao wenyewe sio ya kiwango kinachotakiwa hapo watawezaje kuwahimiza wengine?

Na kazi hii inahitaji kufanywa kwa mapenzi na haiba na upole. Wakati fulani baadhi ya watu wanakuwa wagumu na hivyo unalazimika kwenda tena na tena, mara moja, mbili, tatu, na hata mara nne na kila mara khulka yako wakati wote inahitajika iwe ya mapenzi, wema na upole na haitakiwi dalili yoyote ya ukali/kuchukia ionekane kwenye uso wako.

Hakuna yoyote anayepaswa kufikiri – na wote wanaotoa chanda wakumbuke hili – kwamba mfumo wa Jamaat – nidhamu ya jamaat – inakwenda kwa sababu ya michango yao na hiyo ndio sababu katibu wa fedha anawajia mara kwa mara.

Hii ni ahadi ya Allah ambayo alifanya na Masihi Aliyeahidiwa (a.s) kwamba hakutakuwa na hali ya uhaba wowote wa fedha na mambo yataendelea. Inshallah. Kama alikuwa na hofu yoyote basi ilikuwa ni juu ya kwamba fedha zitatumika ipasavyo!

Kwa fadhili za Allah Aliyetukuka, tunajaribu kuhakikisha kwamba matumizi yanafanywa kwa njia ifaayo kadri iwezekanavyo. Ikiwa katika baadhi ya sehemu uzembe unabainika, fikra za watu hao zinaelekezwa kwenye jambo hili na mfumo wa ukaguzi wa matumizi umewekwa kwa lengo hili hili.

Na hili ni jukumu la Amir wa Jamaat (katika kila nchi) kwamba aweke jicho la umakini katika matumizi na sio kwamba bili yoyote na zote zinazokuja zipitishwe tu moja kwa moja bila ya haja. Fanyeni mfumo wa ukaguzi wa mahesabu kuwa wenye ufanisi na uruhusuni kuenenda kwa uhuru na mamlaka ili kwamba wakaguzi waweze kutenda kazi zao kwa mamlaka kamili na wapewe madaraka yaliyokamilika.

Kuhusiana na matumizi, hebu nimwambie kila mmoja wenu kwamba kuendesha MTA ni gharama kubwa kabisa na maombi tofauti ya kutoa kwa ajili yake hufanywa kwani kwa sasa imesambaa juu ya ardhi yote na satalite tano zinatumika na gharama hizi haziwezi kukidhiwa na michango hii pekee. Fedha kutoka katika bajeti kuu ya Jamaat zinatumika vile vile. Kwa hivyo watu waangalie mahitaji haya pia. Ikiwa watu wanasikiliza hotuba yangu ya siku ya pili ya Jalsa ambayo huitoa hapa Uingereza hapo kila mmoja ataona ni baraka kiasi gani Allah anaziweka katika fedha za Jamaat na ni wa kushanagza kiasi gani ukubwa na ukubwa wa kazi ya Jamaat inavyoendelea kupanuka na kukua.

Kwa fadhili na rehema za Allah matumizi haya yote yanakidhiwa kwa msingi wa kujitolea kifedha kwa wanajumuiya.

**Mbali na mambo hayo niliyokwisha yasema nataka pia kuzielekeza fikra za Jamaat kwenye baadhi ya shughuli za kiutendaji za kila siku.** Kama nilivyosema kabla ni muhimu kwamba watu wasikilize khutba za Khalifa wa zama na maelekezo mengine yanayotolewa nyakati mbalimbali na katika matukio mbali mbali. Wakati viongozi wanapowaelekeza wanajumuiya juu ya mambo haya wao wenyewe pia waonyeshe kuyazingataia.

Ni wajibu sana kwa Amir wa nchi kwamba ikiwa mwongozo fulani umetolewa katika hotuba au ikiwa mafunzo fulani na elimu fulani imeelekezwa anapaswa mara moja kuandika kumbu kumbu yake na kutuma kwa marais wa Jamaat mbalimbali mara moja na kisha jambo hilo lifuatiliwe kwa makini na tathmini ifanyike mara kwa mara kuona kwa kiasi gani hatua zinachukuliwa juu ya jambo hilo. Kwa kiasi utumaji ripoti unavyohusika ni Amir wa Jamaat ya USA tu ndiye anayefanya hivyo mpaka sasa na hutoa ripoti, hivyo na wengine wanapaswa pia kutenda kama hivyo.

Uingereza ni mahali padogo sana na kama kazi itafanywa vizuri katika hili matokeo bora zaidi yanaweza kufikiwa hapa kuliko pengine popote. Halikadhalika ikiwa maagizo yoyote yametolewa na Markaz au kutoka kwangu hayo yanapaswa kupelekwa mara moja kwa jamaat zote kisha kunatakiwa kuwepo na ufuatiliaji wa haya na taarifa zipatikane na zitolewe.

Vile vile Ameer wa kitaifa sio tu achague Maamiri wa mikoa na kisha akae tu na kudhani kwamba Maamiri wa mikoa wanashughulikia kila kitu. Hii haipaswi kutokea. Hii sio namna sahihi ya kutenda mambo. Kwa kadri nilivyoangalia umbali kati ya wanajumuiya na Markaz unaongezeka kwa sababu ya jambo hili. Kwa kweli wanaanza kujisikia kwamba hawawezi kuifikia markaz moja kwa moja – na hapa namaanisha markaz za nchini mwao – hivyo ipo haja ya haraka ya kuzifuta hisia hizi.

Basi hapa (Uingereza) na sehemu nyinginezo pia hadhari ni lazima ichukuliwe na kuhakikisha kwamba angalau mara mbili kwa mwaka kifanyike kikao kati ya Amir na marais na tathimini ifanyike ya kasi ya utekelezaji wa kazi mbalimbali. Wale marais ambao hawatekelezi majukumu yao pamoja na kukumbushwa mara kwa mara taarifa zao zitumwe kwangu. Hili lifanyike pia kwa makatibu wa Fedha, Tarbiyyat na Tabligh. Kama sio mara mbili kwa mwaka basi angalau mara moja kwa mwaka kikao hiki kifanyike na upimaji ufanyike wa kasi yao ya utekelezaji wa kazi. Ikiwa makatibu hawa watakuwa wafanisi na washughulikaji basi hofu na matatizo yanayozikabili idara zingine yatatatuka yenyewe.

Kwa hiyo kuanzia hii leo maamiri wa nchi lazima wapange mipango yao ya namna watakavyoyafikia matawi yote ya Jamaat na kuifanya nidhamu ya Jumuiya itekelezwe kikamilifu na kwa ufanisi. Hili si jambo gumu hata kidogo kwa Uingereza na nchi nyingine ndogo ambamo watu wanaweza kukusanywa Makao makuu kwa urahisi. Nchi kubwa kama USA na Canada zinahitaji kufanya mipango ya njia itakayowezesha kuwepo mawasiliano ya moja kwa moja na kufikia kiwango hiki cha ufanisi na kuhakikisha kwamba matawi yote yanakuwa katika harakati kikamilifu na kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi, na kama inavyohitajika na Jamaat.

**Jambo moja jingine ambalo nimelisema mara nyingi huko nyuma pia ni kwamba wanajumuiya ni lazima watendewe kwa mapenzi na ukaribu na wema.** Mambo niliyoyaeleza katika majlis Shura ni lazima ihakikishwe kwamba yanamfikia kila mtumishi na ofisi ya Tabshir ihakikishe hilo linatendeka.

Kuhusu masuala ya utendaji wa kila siku nataka kusema jambo moja jingine kwamba watendaji wote maofisini ni lazima wajielimishe juu ya kanuni na mahitaji na majukumu na mamlaka ya ofisi walizonazo. Kila matumishi ni lazima ajue haki na wajibu wake.

Mojawapo ya majukumu ya Amir wa nchi ni kwamba wakati amemteua Amir wa Mkoa ni lazima aiarifu Markaz juu ya kazi na mamlaka aliyopangiwa. Hakuna hatua yoyote inayochukuliwa juu ya utaratibu huu mahali popote hivi sasa, kwa kadri ninavyoweza kukumbuka sijapata kupokea barua ikisema kwamba mtu fulani ameteuliwa kuwa Amir wa Mkoa na amepewa mamlaka haya na majukumu haya. Kanuni namba 177 imeandikwa juu ya jambo hili na iko wazi kabisa. Sasa hivi iko haja ya jambo hili na zingatio lazima lifanywe kwenye jambo hili.

Umara (Uongozi) ni lazima ulifanye ni jambo la muhimu kujifunza kanuni Na. 215 hadi 220 katika kitabu cha Kanuni (na Miongozo ya Tahrik Jadid) na muda wote kuziweka akilini na kuzifuata hususan pale maamuzi yanapotakiwa kufanywa juu ya jambo mahsusi.

Kwa mnasaba huu nataka kuwakumbusha Wabashiri pia

*Endelea uk. 9*

# Kila Ahmadiyya atekeleze wajibu wake

*Kutoka uk. 12*

hazitajwi kwa kuzingatia kwamba mafunzo ya kielimu na kimalezi ya wanajumuiya wetu yanahitaji imani hizo zitajwe kwa usahihi na uwazi kabisa.

Mara nyingi inafikiriwa kwamba wale waliozaliwa ndani ya Jumuiya wanayaelewa masuala haya moja kwa moja na pia wanaelewa lengo la kutumwa kwa Masihi Aliyeahidiwa a.s. duniani na ni kwa nini akubaliwe. Wale waliojiunga wenyewe na Jumuiya bila shaka huyaelewa mambo hayo kwani hujiunga baada ya kusoma masuala haya. Lakini wale ambao kama nilivyosema (hata kama wamezaliwa ndani ya Jamaat) hawachangamki na hawashiriki kwenye Ijtimai na hawafiki kwenye Jalsa – na watu kama hao hupatikana katika kila nchi ambapo Jumuiya ipo, iwe ni wachache au wengi lakini kundi hilo lipo – na hivyo ni muhimu kuelekeza fikra zetu kwao kwa kuwajali na kuwakusudia.

Na kwa ajili hiyo Majlis Khuddamul Ahmadiyya na Lajna Imaillah zinahitajika kuelekeza fikra zao na kupanga mipango na kuitekeleza kwa ajili ya kukabiliana na masuala haya. Hivyo hivyo utaratibu wa kijumuiya nao unahitajika kuwaelekea watu kama hao na kupanga mipango kwa ajili ya kuwarekebisha badala ya kuwasukumia pembeni au kuwadharau kwa madai kwamba hawawezi kurekebishika, isipokuwa kama wenyewe watamke wazi kwamba hawana uhusiano tena nasi.

Lakini hata kama wafikie kusema hivyo, uongozi wa Jumuiya uzipatie taarifa tanzeem kwa sababu wakati mwingine kauli kama hizo huweza kutolewa kutokana na ukali wa viongozi wa juu. Ni jambo linalowezekana kwamba watu hawa wanaweza kuzingatia iwapo nasaha zitatolewa na watu wa rika lao au umri wao au wanaofanana nao kikazi n.k. na hivyo Tanzeem zinaweza kuwafikia watu hawa na kuwarekebisha.

Mahala popote ambapo njia hii imeshikwa tumeweza kuona mafanikio kwa fadhili za Allah. Katika baadhi ya sehemu wapo makatibu wa malezi ambao wameandaa mipango kwa kuzingatia saikolojia na mitazamo ya watu hawa na mipango hiyo imezaa matunda mazuri na kuleta athari na wamepata majibu mazuri kutoka kwa watu hawa ambao walishaachana na Jumuiya kiasi hicho.

Katika hali yoyote iwayo juhudi zetu zinahitajika kuhakikisha kwamba tunamuokoa kila Ahmadiyya kwa kadri inavyowezekana na sawa na uwezo wetu. Hili ni jukumu la kila kiongozi na kila Mbashiri na kila mwalimu wa kila ngazi ndani ya Jumuiya na Tanzeem pia – bali hasa ni jukumu la kila mmoja wetu.

Hivyo baada ya utangulizi huo wa msingi, sasa nitafafanua jambo la kwanza ambalo kila Ahmadiyya anatakiwa alielewe nalo ni: ***Ni lipi lengo la kutumwa kwa Masihi Aliyeahidiwa a.s. na ni kwa nini tunalazimika kumkubali na kutangaza madai yake?*** Kwa ajili ya hili, nafikiria ni bora nijibu kwa kutumia maneno ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. yeye mwenywe.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema:

*Nimetumwa ili kwamba nirejeshe tena heshima iliyopotea ya Mtukufu Mtume s.a.w. na kuionesha dunia ukweli uliomo ndani ya Kurani Tukufu na haya yote yanatendeka ingawaje wale ambao macho yao yamefunikwa na kizibo hawawezi kuona jambo hili, ingawaje mwendeleo huu umekuwa bayana na unatoa mwanga wake kama jua na watu wengi ni mshahidi wa ishara na miujiza ionyeshwayo ili kuuunga mkono mwendeleo huu kiasi hiki kwamba kama ikusanywe pamoja idadi yao itakuwa kubwa kiasi cha kulishinda jeshi la mfalme yeyote juu ya uso wa ardhi.*

Masihi Aliyeahidiwa s.a. anaendelea kusema: *"Kuna namna nyingi ambazo ukweli wa mwendeleo huu unaweza kuthibitishwa kiasi kwamba haiwezekani kuzitaja zote, Kwa sababu Islam ilidhalilishwa kwa njia za ukatili na dhuluma sana, hivyo Mwenyezi Mungu amedhihirisha ukuu na heshima ya mwendeleo huu kwa kiwango kilicho sawa na idhilali na udhalimu uliofanywa dhidi ya Islam.*

Sasa jambo hili halikuishia wakati wa Masihi Aliyeahidiwa tu. Jinsi Masihi Aliyeahidiwa (a.s) alivyouelezea na kusisitiza ukuu na ubora wa Mtume s.a.w. na kufafanua na kudhihirisha ukweli wa Kurani Tukufu katika zama zake kupitia maandishi yake na hotuba zake – jambo hilo linaendelea kuleta atahri zake hadi sasa. Nimeendelea kutaja mara kadhaa jinsi wakati watu wanapoelezewa kweli hizi wanavyojisikia kulazimika kukubali kwamba haya ni mambo makuu na kama huu ndio mfano mwema wa Mtukufu Mtume s.a.w. na mafundisho yake basi kwa hakika wao ni wakosefu.

Siku zilizopita niliwahi kutaja mfano wa mpinzani mmoja mkubwa wa Islam wa huko Canada ambaye naye alichapisha kwenye gazeti lake vikatuni vile vilivyochapishwa Denmark dhidi ya Mtume s.a.w. wakati aliposikiliza maelezo yangu kuhusu uzuri wa mafundisho ya Islam, alijisikia kulazimika kuandika kwenye gazeti lake kwamba baada ya kumsikiliza Kiongozi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya ameelewa ukweli. Na aliendelea kuandika kukubali kwamba hapo kabla alikosea.

Vile vile nilieleza kwenye hotuba zangu zilizopita kwamba huko Amerika mwanasiasa mmoja mashuhuri aliwahi kuitusi Islam kwenye redio yake kuhusiana na sala ya Ijumaa. Redio yake inasikilizwa na malaki ya watu. Kufuatia matusi hayo kijana mmoja wa Jumuiya aliandika makala akielezea ukweli wa mafundisho ya Islam kuhusiana na sala ya Ijumaa na makala hiyo ikatumwa pia kwenye tovuti yao.

Kisha mwanasiasa huyu aliandikwa barua na kuelezwa kwamba alichowahi kukiongea hakikuwa sahihi na mtu huyu kama nilivyosema ni mtu mashuhuri na anajulikana sana na kisha akaombwa kutupatia nafasi kwenye redio yake naye akafanya hivyo. Hili bila shaka linadhihirisha asili yake njema.

Basi kijana wetu yule alihudhuria kwenye kipindi hicho na kwa fadhili za Allah alitoa maelezo mazuri kuhusu Ijumaa na Kurani tukufu kwa ujumla na baada ya kusikiliza kwa makini yule mwasiasa alikiri kwamba alikuwa amekosea. Kipindi hiki kilisikilizwa na maelefu ya wasikilizaji.

Wasikilzaji wote walikiri kwamba ni kwa kupitia Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya kwamba wamepata kujua uzuri wa mafundisho ya Islam. Na haya yote yanatokea na yanawezekana kwa sababu ya kweli zile ambazo Masihi Aliyeahidiwa a.s. amezifafanua na kuzieleza kwetu, na ni kwa sababu hiyo Allah Aliyetukuka alimtuma duniani – ili kwamba aieleze dunia kwa usahihi nafasi na hadhi ya Mtukufu Mtume s.a..w na kuweka bayana ukweli wa Kurani Tukufu.

Kwa hiyo jambo hili ndilo linaloendelea kupitia kwa Masihi Aliyeahidiwa (a.s), na kwa namna ile ile aliyoieleza, adhama ya Mtume Mtukufu s.a.w. na kweli za Kurani Tukufu na haiba ya Islam zinatambulika duniani kupitia kazi zake na elimu aliyoileta duniani. Kwa hiyo hakuna sababu ya sisi kuzama katika dhana za kujiona dhalili (duni) mbele ya watu wengine kwa namna yoyote na wadogo miongoni mwetu hawahitaji kumuogopa yeyote na wajiamini. Popote vijana wa Jumuiya wanapokuwa wachangamkaji wanaweza kuziba midomo ya watu wote wanaojaribu kuiabisha Islam au mwanzilishi Mtukufu s.a.w. au kitabu Kitukufu.

Kisha ni muhimu kwetu sote kutambua kwa nini ni jambo la lazima kwa kila mmoja wetu kuupokea na kuumini ukweli wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. Watoto wadogo wa miaka kama 13 na 14 wanauliza maswali haya na wazazi hawatoi majibu sawa sawa.

Hebu tena nijibu kwa maneno ya Masihi Aliyeahidiwa (a.s). Haya ni maelezo ya kina juu ya swali hili na watumishi wa tandheem wanaweza kuyachapisha kwa ukubwa mbalimbali na kujipatia muongozo zaidi kutokana nayo.

Siku moja Mamulla walimuuliza Masihi Aliyeahidiwa (a.s) kwamba sisi tunasali, tunafunga saumu, tunaiamini Kurani Tukufu na Mtume s.a.w. pia, sasa kuna haja gani juu ya kukuamini wewe na kukufuata?

Masihi Aliyeahidiwa (a.s) alijibu: *"Tazameni, kama ambavyo mtu angedai kuwa amemwamini Allah na Mtume Wake s.a.w. na Kitabu Chake lakini pamoja na hayo akashindwa kutekeleza matakwa ya imani – sala, saumu, Hajj, Zakat, kushikamana na wema na utawa – na kuzifuata amri zile za imani zinazohusikana na kufikia utakaso wa nafsi ya mtu na kuachana na kuepukana na mabaya yote na mwelekeo wowote wa kutenda dhambi na kuenenda katika njia zote zinazompeleka mtu kwenye mwelekeo wa kutenda mema – ikiwa mtu kama huyo ataachana na miongozo yote hii na haiheshimu mtu kama huyo hana haki ya kudai kwamba yeye ni Mwislamu…"*

Masihi Aliyeahidiwa (a.s) amesema kwamba mtu anayedai kwamba amesilimu lakini hafuati mafundisho ya Islam na haepuki maovu na hatendi mema, mtu kama huyo hana haki ya kujiita mwislamu.

Masihi Aliyeahidiwa (a.s) ameendelea kusema:

*"Na haiwezi kusemwa kwamba mtu kama huyo amepambwa na mapambo ya imani. Hali kadhalika mtu ambaye hamkubali au kumwamini Masihi Aliyeahidiwa (a.s) au haoni haja ya kumuamini Masihi Aliyeahidiwa (a.s) mtu kama huyo pia anashindwa kuelewa na yuko gizani kabisa kuhusu ukweli wa Islam au haja ya Unabii na lengo la kuja kwa manabii wa Mungu. Na mtu kama huyo kwa kweli hawezi kuitwa Muislamu wa kweli au mfuasi wa kweli wa Mungu na Nabii Wake Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w. Kwa sababu kama mabavyo Allah ametuma amri zake kupitia Mtume Mtukufu s.a.w. katika Kurani Tukufu, kwa njia hiyo hiyo katika siku za mwisho amebashiri wazi wazi kabisa ujio wa Khalifa wa mwisho na wale ambao hawatamwamini au watakaojitenga naye wameitwa waasi. Hakuna tofauti kati ya Kurani Tukufu na Hadees kuhusu hili. Maneno ya Hadees ni maelezo ya yale yaliyomo katika Kurani Tukufu. Neno lililotumika katika Kurani Tukufu ni Khalifa na neno hili hili linatajwa katika Hadees kuwa ni Masihi Aliyeahidiwa (a.s). Hivyo mtu ambaye kumuhusu yeye ahadi imefanywa ndani ya Kurani Tukufu kwa fasaha ya kiasi hiki atakuwa ni Musialmu wa aina gani huyo ambaye anauliza iwapi haja ya kumpokea mtu huyu pale anapotokea?"*

Masihi Aliyeahidiwa (a.s) anasema kwamba: *"Allah amerefusha kipindi cha ujio wa Khalifa mpaka siku ya mwisho. Na hii ni sifa ya Islam kwamba kwetu sisi msaada na mwongozo mpya na kwa ajili ya kubaki na uhalisia mujadidina wameendelea kuja na wataendela kuja katika mwanzo wa kila karne. Tazama Allah Aliyetukuka amemfananisha Mtume Mtukufu s.a.w. na Musa a.s.*

Hapa nataka kusahihisha jambo moja ambalo watu wanalikosea kuhusiana na suala na Mujadideen – wasahihishaji – na wanauliza kwamba ikiwa wataendelea kuja, basi watakuwa na nyadhifa gani? Makhalifa ndio wao watakaokuwa Mujadideen – wasahihishaji. Tayari nilishawahi kutoa hotuba ya kina juu suala hili na kumbukumbu zaweza kuchukuliwa kwenye hotuba hiyo.

Vile vile Masihi Aliyeahidiwa (a.s) ameliangazia swala hili kwa undani kabisa na yapo marejeleo ya kutosha katika Jumuiya juu ya swala hili.

Masihi Aliyeahidiwa (a.s) amesema: *"Tazama Allah Aliyetukuka Amemfananisha Mtume Mtukufu s.a.w. na Musa a.s. kama ambavyo iko dhahihiri kwa matumizi ya neno 'kama'. Hadhrat Issa a.s,. Yesu, alikuwa Khalifa wa mwisho wa silsila ya Musa kama ambavyo mwenyewe amepata kusema 'mimi ni tofali la mwisho!"*

*Kwa namna hiyo hiyo kwa ajili ya kuilinda na kuitunza silsila ya Muhammad s.a.w. Makhalifa wameendelea kuja na wataendelea kuja hadi siku ya mwisho na kwa namna ile ile Khalifa wa mwisho wao aliitwa Masihi Aliyeahidiwa.*

*Na si hivyo tu, kwamba jambo hili lilitajwa kwa namna ya kawaida, la hasha, bali kinyume chake dalili za kuja kwake zilielezwa kirefu sana katika sahifa zote za kimbingu. Katika Taurati na Injili na Hadithi na Kurani Tukufu yenyewe ishara za kuja kwake zimeelezwa. Na watu wote, Wakristo, Wayahudi na Waislamu wanasubiri ujio wake na wanaamini jambo hili.*

*Kumkataa yeye hakuwezi kwa namna yoyote kufikiriwa kuwa ni sehemu ya Islam. Na kisha tunapofikiria kwamba yeye ni mtu yule ambaye kwa ajili ya kumsaidia, Allah ameonyesha ishara katika mbingu na ardhi, kwa kusaidia madai yake tauni iliteremshwa na kwa kumsaidia yeye ishara za kupatwa kwa mwezi na jua zilionyeshwa katika nyakati zilizobashiriwa. Hivyo inawezekanaje mtu kama huyo ambaye kwa kumshuhudilia yeye mbingu na rdhi vimetoa ushahidi, anaweza kufikiriwa kuwa mtu wa kawaida ambaye kumkataa au kumkubali kunaweza kudhaniwa kuwa sawa tena hakutoleta athari yoyote? Na watu wanaomkataa waendelee kudhaniwa Waislamu na wapendwa wa Mungu? Bila shaka hapana!*

Masihi Aliyeahidiwa (a.s) anaendelea kusema:

*"Kumbukeni kwamba ishara zote zilizotabiriwa kumhusu yule aliyeahidiwa zimekwisha timia na aina zote za machafuko na maovu yameifunika dunia. Watawa na wanazuoni bila ya shaka walibainisha zama hizi – karne ya 14 – kwamba ndizo zama ambazo Masihi Aliyeahidiwa (a.s) alikuwa atokee."*

Masihi Aliyeahidiwa (a.s) anaendelea kusema:

*"Hata baada ya ushahidi huo bayana wa idadi kubwa ya watawa na wanazuoni wa Kiislam, mtu bado ana shaka, mtu kama huyo ageukie katika kuisoma Kurani Tukufu kwa makini na kutafakari, yaliyomo katika sura Nur. Tazama kama ambavyo miaka 1400 baada ya Musa a.s. Isa a.s. alikuja, hivyo kwa mfanano huo miaka 1,400 baada ya Mtume Muhammad s.a.w., Masihi Aliyeahidiwa (a.s) ametokea na kama ambavyo Yesu a.s. alikuwa ndio Khatamul Khulafaa wa silsila ya Musa a.s. ndivyo ambavyo Masihi Aliyeahidiwa (a.s) atakavyokuwa Khatamul Khulafaa wa silsila ya Muhammad s.a.w."*

Masihi Aliyeahidiwa (a.s) amesema mimi ni Khalifa wa milenia ya mwisho – wote watakaokuja sasa watakuja chini yake. Hivyo Masihi Aliyeahidiwa (a.s) ambaye alikuwa atokee katika karne ya 14 kwa kutimiza bishara zote kwa hakika ni Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. mwenyewe na ni muhimu sana kwamba kila Muahmadiyya asome vitabu vya Masihi Aliyeahidiwa (a.s).

Wale ambao hawawezi kusoma Kiurdu ikiwa wanaweza kusoma Kiingereza au lugha yoyote ile katika nchi ambamo wanaishi vipo vitabu vya kutosha vinavyopatikana katika lugha nyingi ambamo lengo la kutokea kwa Masihi Aliyeahidiwa (a.s) limeelezwa kwa upana mkubwa na kwa nini ni lazima kwamba tumpokee na kuukubali ukweli wake.

Kila mmoja anahitaji kuzielewa imani zake na misingi yake vyema na kuwa imara. Ongeeni na wale wanaoleta upinzani na kutoa lawama. Wajibuni wote. Mkifanya matayarisho yanayohitajika mtajifunza ninyi wenyewe na mtaweza kutoa majibu vile vile.

Kupeleka mbele malengo haya, ni lazima, mbali na juhudi ambazo Waahmadiyya binafsi ni budi wazifanye, Jamaat na Tanzeem pia ziandae mipango yao kuhakikisha kwamba taarifa hii, elimu hii, inamfikia kila mwanajumuiya ili kila mmoja atambue lengo la kuja kwa Masihi Aliyeahidiwa (a.s) na kwa nini ni lazima kwamba tumpokee na kuukubali ukweli wake.

Kwa hiyo hili ni jambo la muhimu linalohusu imani zetu. **Sasa nataka kugeukia kwenye jambo la pili linalohusu malezi yetu. Hili linahusu mahusiano baina ya wanajumuiya na Ukhalifa.** Na kuhusiana na hili inabidi kuitaja Muslim Television Ahmadiyya MTA – ambayo Allah ametupatia ili kulipeleka mbele lengo hili. Halikadhalika tunayo tovuti ya **Alislam.org.** Kwa hivyo inapaswa kuona ni dhamira zetu na jitihada zetu kuhakikisha kwamba kila mwanajumuiya ameunganishwa na nyenzo hizi kwa kadiri inavyowezekana na mfumo na Nizam ya Jamaat na shughuli za watendaji mbalimbali wa Tanzeem lazima zielekezwe katika lengo hili.

Kuna idadi kubwa ya Waahmadiyya – waaminifu na watiifu ambao wanakuja katika msikiti huu wao wenyewe na kusikiliza khutba na kuna wengi ambao katika sehemu mbalimbali za dunia kupitia MTA husikiliza khutba na hufanya hivyo bila kukosa – kwa hakika wako baadhi ambao husikiliza khutba hizi mara mbili au tatu. Hata hivyo ipo idadi fulani ya watu ambao hawasikilizi. Hapa hapa Uingereza wapo watu ambao hawasikilizi khutba, na wala hawaangalii vipindi vingine na vile vile hawashiriki katika hafla mbalimbali (za Jamaat).

Katika Jamaat fulani idadi kubwa ya watu walifanya mambo kinyume na kabisa na mafundisho na mwenendo wa kijumuiya na

***Endelea uk. 10***

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

# MapenziyaMungu

Shawwal 1434 AH | Agosti 2013 | Zahoor 1392 HS

**Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w**

**Imesimuliwa na Hadhrat Ibn Abbas r.a. kwamba Mtume s.a.w. alisema: Yule aonaye ndani ya amiri kitu anachochukia, basi asubiri (wala asiachane na Jumuiya), kwani anayetengana na Jumuiya (kiasi kidogo sana) sawa na shibiri moja atakufa kifo cha kijinga (Bukhari). (*Bukhari*)**

# Kila Ahmadiyya atekeleze wajibu wake - Khalifa Mtukufu

**Na Mwandishi wetu**
**Dar es Salaam**

Siku kadhaa zilizopita nilikuwa na mazungumzo na baadhi ya watendaji wa Jumuiya na hapo nikabainikiwa kwamba kuna haja ya kutoa ufafanuzi juu ya masuala kadhaa. Jambo hili linahitajika mno kwa ajili ya kundi fulani la wanajumuiya. Kisha kuna baadhi ya mambo ambayo yanahitaji kutolewa ufafanuzi kwa ajili ya viongozi wa Jumuiya.

Mambo ninayotaka kuyazungumza ni muhimu sana, kwa Jumuiya zote duniani kama yalivyo muhimu kwa Jumuiya ya hapa (Uingereza). Pia masuala haya yanahitajika sana na kizazi chetu kipya cha Kiahmadiyya na kwa wale pia ambao si wachangamkaji na ambao hawajishirikishi na kazi za Jamaat.

Masuala nitakayoyaweka mbele ya kila mmoja wenu ni mambo ambayo kwa kawaida hayazungumzwi bayana na kwa undani wake. Wabashiri, waalimu na washika nafasi za ofisi mbalimbali pia hawayafafanuwi mambo haya kwa kiasi kinachotakiwa yafafanuliwe na matokeo yake masuala mengi huibuka ndani ya vichwa ya baadhi ya ya wanajumuiya – ingawaje nao hawayaulizi maswali hayo. Hali hii hasa inawakabili vijana. Wao huhisi kwamba walio wakubwa au wazazi wao au washika nafasi za kiofisi watahesabu kuulizwa maswali hayo kuwa ni jambo baya au kwamba wao vijana watajiingiza kwenye matatizo ya bure.



*Kiongozi wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya duniani, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (a.t.b.a)*

Uhakika wa mambo ni huu kwamba, walitakiwa wawe na mahusiano mazuri nao ambayo yangewawezesha kuuliza maswali hayo kwa wabashiri wao au viongozi wengine wa Jamaat au angalau viongozi wa tanzeem zao. Jambo hilo lingewaongezea zaidi ufahamu wao na kuondoa mashaka na uelewa mbaya.

Pia wangeweza kuniandikia mimi, na baadhi yao kutoka nchi za nje wananiandikia, na kutoka hapa pia wananiandikia na wanafanya hivyo wakibaki kwenye mipaka inayotakiwa na heshima inayohitajika kwenye kutofautiana, na maswali yao hujibiwa ipasavyo.

Kwa vyovyote viwavyo inaonekana ni jambo lililo wazi kwamba baadhi ya washika nafazi za kiofisi hawaelewi majukumu yawapasayo sawa na ofisi zao na hivyo hawatimizi ipasavyo majukumu ya ofisi zao.

Mambo ninayotaka kuyazungumza yanahitaji kuwa na elimu ya msingi wa imani zetu na pia yanahitaji kuelewa kwa nini tunalazimika kubaki kwenye imani na taratibu maalum. Pia tunapoambiwa kufanya jambo fulani ni lazima tuelewe kwa nini tunalazimika kufanya jambo hilo na kwa nini kufanya mambo hayo ni kitu cha lazima kwa Mwahmadiyya.

Kwa mfano, kujitolea mali ambako tunatakiwa kukutekeleza, watu wanahitaji kujua masuala haya. Kisha kuna vipengele vya majukumu ya kiofisi ambayo yanapelekea kutimiza majukumu ipasavyo na hivyo viongozi wanahitaji kuelewa ni kwa vipi wataweza kutekeleza majukumu hayo. Viongozi pia wanahitaji kujua mipaka ya uongozi wao. Hivyo nitajaribu kuwaelekeza kwenye masuala haya yote.

Jambo la kwanza linalohitajika kutajwa linahusiana zaidi na imani zetu na ni muhimu kabisa kwamba kila Ahmadiyya ni lazima azijuwe hizo na bila shaka hizi zimeendelea kutajwa kila mara lakini hazitajwi kwa nguvu na msisitizo ule unaohitajika au

*Endelea uk. 11*

# Kipimo cha kukubaliwa saumu zetu tunacho wenyewe

**Na Abdillah Kombo, Kitunda.**

Kwa fadhila za Mwenyezi Mungu Waislam duniani kote waliweza kwa mara nyingine tena kutimiza moja ya nguzo kuu kabisa ya kiimani katika Islam ambayo ni kufunga saumu ya Ramadhani. Na kama ilivyo ada, kila baada ya ibada hiyo, Waislamu Duniani kote hushiriki katika ibada ya Siku ya Idd (Maarufu kwa jina la Idd –ul –Fitri). Katika kusheherekea Siku hiyo, Waislam hufanya mambo mbalimbali ya ibada ili kuwazidishia ukaribu wao na Mwenyezi Mungu. Tawi la Jumuiyya ya Waislam Waahmadiyya la huko Kitunda katika kuadhimisha Siku ya Idd walifanya Baraza la Idd katika Msikiti wa Jumuiyya huko huko Kitunda Wilaya ya Ilala Mkoani Dar Es Salaam. Katika kikao hicho hutuba kadha za Malezi na Mahubiri kwa washiriki zilitolewa ili kufikia adhma ya Sherehe za Idd.

Hutuba iliyokonga Mioyo ya washiriki wengi ni ile iliyotolewa na Mwalim Ramzan Fazal, Katibu Wasia Taifa, iliyokuwa na anuani iliyosema kuwa "Kukubaliwa kwa Saumu ya Ramadhani". Mwl. Ramzan alianza hutuba yake kwa kusoma sehemu ya aya ya Sura 5 aya ya 28 sehemu inayosomeka kama "Mwenyezi Mungu Huwapokelea wamchao tu". Kisha alifafanua maada yake kwa kusema 'Maada niliyopangiwa inakusudia katika kutuwezesha kutambua kipimo cha kutuwezesha kujua kuwa Saumu tulizokuwa tukifunga je zimekubaliwa na MwenyeziMungu aulaa. Hakika mengi yanaweza kusemwa ili kutufahamisha kipimo hicho mimi nitatoa vigezo vitatu vya muhimu katika kupimia kukubaliwa huko kwa Saumu ya Ramadhani'.

KUSUDIO LA KUFUNGA SAUMU:

Kigezo cha kwanza kimsingi kilikuwa ni sawa na kusudio la jambo lenyewe. Kama alivyosema Mwenyezi Mungu katika Qurani Tukufu kuwa "ENYI MLIOAMINI MMELAZIMISHWA KUFUNGA SAUMU KAMA WALIVYOLAZIMISHWA WA KABLA YENU ILI MPATE KUMCHA MUNGU" (2:184). Katika aya hii, kusudio la amri ya kuwataka waislam wafunge saumu ya Ramadhani imeelezwa mwishoni mwa aya kuwa "Ili mpate kumcha Mungu". Kumbe lengo la kujinyima kula na kunywa na baadhi ya mambo ambayo yanaruhusiwa katika siku za kawaida kuto yafanya wakati wa kuanzia mawio mpaka machweo ya jua ni kutafuta Radhi ya Mwenyezi Mungu yaani Kumcha Mwenyezi Mungu.

Hivyo kama huu ndio msingi wa

*Endelea uk. 8*

# Ansarullah waambiwa wafanye kazi za Jumuiya kama nyuki

**Na Katibu wa Habari**
**Ansarullah**

Mfululizo wa Semina ya viongozi wa Answarullah kwa kuwaweka katika hali ya kuelewa mambo ya Tanzim, bado unaendelea hadi pale Majlis Answarullah Ahmadiyya Tanzania itakapojiridhisha kwamba sasa wanachama wake wote wanaelewa wajibu wao. Ukiachia Semina iliyofanyika kule Bukoba Mkoa wa Kagera, Newala Kanda ya Kusini, Lakini vile vile kwa fadhili za Mwenyezi Mungu, Semina ya tatu imefanyika kule Ifakara, Wilaya ya Kilombero Mkoa wa Morogoro. Semina hiyo imefanyika mnamo tarehe 24 - 25 ya Mwezi Agosti 2013. Kutoka Makao Makuu, Sadr Sahib Muadhamu Inayatullah S. Nakuchima alipeleka huko wakufunzi wanne



*Abdallah Nassor*
*Naibu Sadr Ansarullah*

wakiongozwa na Naib Sadr - I Bwana Abdullah bin Nasoro.

Naam, kwanza Semina hii ilipangwa ifanyike kwenye shule moja ya kule ambako viti, meza na ubao vingepatikana kiurahisi zaidi. Kumbe kulikuwapo Agizo la Mkuu wa Wilaya hiyo likikataza shughuli na mikutano yoyote ya kidini, isifanyike kwenye maeneo ya shule za serikali. Lakini ni kweli kwamba pawapo watu aghalabu kuharibika mambo kwa juhudi ya Bwana Mohamedi Henji ambaye ndiye Zaim wa Ifakara akishirikiana na viongozi wa Jumuiyya ya huko, mahala pengine pa kuendeshea Semina hiyo palipatikana. Ni kwenye ukumbi wa Ofisi ya CCM ya Kapalapala Ifakara. Answarullah 23 walihudhuria Semina hii na viongozi 5 wa Serikali na wa vyama mbalimbali vya siasa kijijini hapo walialikwa. Mmoja kati ya

*Endelea uk. 9*